# Nipashe

Alhamisi Aprili 6, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581272

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11


SUPA JACKPOT

TZS. 1,099,164,188

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




## Sabaya ahukumiwa kifungo cha nje mwaka

UKURASA 3

## Vyama sita vyalamba bilioni 17/- za ruzuku

UKURASA 3

# Kikokotoo mafao bado ni mwiba kwa watumishi



• **Wamlilia** Mwigulu, atoa neno la matumaini...*Ukurasa 2*



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kulia), akipokea tuzo maalum ya 'VIP Global Water Changemarkers', kutoka kwa Rais mstaafu na Mwenyekiti wa Bodi ya Ushirika wa Maji Duniani na Kusini mwa Afrika, Dk. Jakaya Kikwete, katika hafla iliyofanyika Ikulu, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## BRELA na DSE zakwaa kigingi kuhamisha hisa Tanga Cement

UKURASA 2


MIAKA 59 YA MUUNGANO

TOLEO MAALUM

26TH APRIL TANGANYIKA & ZANZIBAR



Kampuni ya the Guardian Limited, Wachapishaji wa Magazeti ya the Guardian na Nipashe, inawakaribisha wadau wote wa maendeleo kutoa salaam za pongezi wakati tunaadhimisha miaka 59 ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Toleo hili litachapishwa tarehe 26 Aprili, 2023 kwenye Magazeti ya Guardian na Nipashe.

The Guardian Nipashe

Kwa mawasiliano zaidi, Tupigie +255 677 020 701

Email: advertise@guardian.co.tz or Visit us at The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Opposite ITV / Radio One, Dar es Salaam

Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com



**MICHEZO** SIMBA YAWAPIGA 'STOP' AKPAN, OKWA, IHEFU UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Kikokotoo mafao mwiba kwa watumishi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KIKOKOTOO cha mafao kimeendelea kuwa mwiba kwa watumishi wengi baada ya wafanyakazi wa Wizara ya Fedha na Mipango kumwangukia Waziri wao, Dk. Mwigulu Nchemba, wakimwomba afikishe kilio chao serikalini ili kifanyiwe marekebisho.

Kilio hicho cha wafanyakazi kiliibuka jana baada ya Dk. Nchemba kufungua mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Fedha na Mipango unaoendelea jijini hapa.

Baada ya kufungua mkutano huo, waziri huyo alitoa fursa kwa washiriki kwa yeyote mwenye jambo lake ambalo angependa kuzungumza mbele yake ili atoe dukuduku lake.

Kutokana na fursa hiyo, mmoja wa wajumbe wa baraza hilo, Consolata Maimu, alinyoosha mkono na kupatiwa kipaza sauti na kujitambulisha, hatimaye kutoa malalamiko yake kuhusu kikokotoo kipya cha mafao kwa watumishi wa umma.

"Mweshimiwa Waziri, malalamiko yangu ni kikokotoo cha mafao kwa watumishi wa umma bado ni mwiba mkali kwetu. Hivi sasa ukiangalia kwa mtumishi ambaye amefanya kazi kwa miaka 37 na akaishia kwenye mshahara wa Sh. milioni 1.6, anapaswa kulipwa mafao kwa mkupuo Sh. milioni 62 wakati kama angelipwa kwa mkataba wa kwanza alioajiriwa nao, angetakiwa kupata kwa mkupuo wa Sh. milioni 126.

"Sasa kwa nini sisi ambao tunastaafu hivi sasa kulipwa kwa mkataba huu mpya wakati tumeajiriwa na mkataba ule wa awali kabla ya kikokotoo hiki? Tunakuomba mheshimiwa suala hili utufikishie ngazi za juu za serikali ili waangalie upya namna ya kurekebisha hiki kikokotoo kinachotumika sasa,"alisema.

Akijibu hoja hiyo, Dk. Nchemba alisema hivi karibuni watakuwa na kikao baina ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Ofisi ya Waziri Mkuu na atatumia nafasi hiyo kufikisha kilio hicho cha watumishi kuhusu kikokotoo.

"Hivi karibuni tutakuwa na kikao na wenzetu wa utumishi na mwenye wafanyakazi Ofisi ya Waziri Mkuu, hivyo tutalizingatia tutakapokutana na wenzetu," alisema Dk. Nchemba.

Awali, akifungua mkutano wa baraza hilo, aliwataka watumishi wa wizara kuwa mfano katika matumizi bora ya fedha na kubana matumizi ya bajeti wanayopangiwa.

"Hiki ni kakao cha kujitathimini. Mara nyingi tumekuwa tukiziambia wizara zingine tunapozipatia fedha kuwa zinapaswa kutumia vizuri fedha za umma ili ziwe na tija lakini sisi ndio tunapaswa kuwa wa mfano katika matumizi bora ya fedha. Wizara yetu ndiyo taswira ya nchi yetu hata maandiko matakatifu yanasema ilipo hazina yako ndipo ulipo moyo wako," alisema.

Aidha, aliwaagiza maofisa madawati wa wizara hiyo kuchangamkia fursa za ufadhili wa masomo nje ya nchi ambazo kwa hivi karibuni Tanzania imekuwa ikikosa watu wa kujijaza nafasi hizo.

"Unapokwenda nje unakutana na watu wa mataifa madogo lakini Mtanzania humkuti na nafasi hizi zinatangazwa. Shida ni maofisa madawati wengine wakizipokea fursa hizo hawataki wengine wanufaike nazo, hivyo badilikeni. Ili fursa zote tuzipate na vijana wetu wenye sifa waende kusoma, msiwe maofisa dawati wa safari peke yake," alisema.

Alisema serikali inaendelea na mikakati yake ya kuboresha maslahi ya watumishi na hadi sasa imeshalipa malimbikizo ya madai ya zaidi ya Sh. bilioni 34 na kutoa mikopo ya usafiri Sh. bilioni 79.




Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari wanawake Tanzania (TAMWA), Dk. Rose Reuben (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu siku ya uhuru wa vyombo vya habari duniani inayotarajiwa kufanyika kitaifa Mei 3, mwaka huu Zanzibar. Wengine ni Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Habari MAELEZO, Rodney Thadeus (kushoto) na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Ofisi ya Umoja wa Mataifa nchini, Nancy Angulo. **PICHA: JENIFER GILLA.**

## BRELA, DSE zakwaa kigingi kuhamisha hisa Saruji Tanga

**Na Kulwa Mzee**

BARAZA la Ushindani Tanzania limezuia kwa muda Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na Soko la Hisa Dar es Salaam kuendelea na mchakato wa kuhamisha hisa kutoka Kampuni ya Saruji Tanga kwenda kampuni ya Scancem International DA (SID).

Uamuzi huo ulitolewa hivi karibuni mbele ya Mwenyekiti Jaji Salma Maghimbi akiwa na wajumbe, Dk. Onesmo Kyauke na Dk. Goodwill Wanga.

Mwombaji, Peter Hellar aliwasilisha maombi dhidi ya Tume ya Ushindani (FCC), Scancem International DA, Fayaz Bhojani, William Erio na Hakan Gurdal. Kwa mujibu wa vyanzo vya ndani, Scancem ndiyo mmiliki wa kampuni ya Saruji ya Twiga ikiwa na asilimia 67.25 huku asilimia 32.5 zikimilikiwa na watu wengine.

Mwombaji aliwasilisha maombi katika Baraza la Ushindani Tanzania yakiwa na milengo miwili, kwanza yasikilizwe upande mmoja kwamba Baraza la Ushindani Tanzania lizuie kwa muda uunganishaji wa kampuni mbili kwa maana ya kwamba hisa za Kampuni ya Tanga Cement ambazo ni asilimia 68.33 zihamishiwe Kampuni ya Scancem International DA.

Mwombaji anadai kama uunganishwaji umeshafanyika au ulishafanyika wakati wa usikilizwaji wa maombi ya msingi, amri itolewe dhidi ya BRELA na Soko la Hisa Dar es Salaam kusajili au kutekeleza kwa vitendo au hatua ambazo zingefuata katika kukazia amri ya kuunganisha kampuni.

Mlengo wa pili, maombi yasikilizwe pande zote mbili na Baraza litoe amri ya zuio kwa pande zote mbili kuzuia uunganishwaji wa kampuni hizo kama ilivyotangazwa na Tume ya Ushindani katika gazeti la Daily News la Februari 11, 2023 wakati wa kusikiliza maombi ya kukiuka amri ya Baraza dhidi ya walalamikiwa.

Katika uamuzi wake, Baraza lilisema baada ya kupitia hoja zilizowasilishwa na waombaji wanajua kwamba zuio lililokuwa linazuia uunganishwaji wa kampuni hizo la Septemba 13, 2022 hawawezi kukataa kwamba limewashangaza.

Jaji Maghimbi alisema chini ya miezi mitano tangu walipotoa uamuzi, maombi mengine ya aina hiyo hiyo yamepelekwa na mlalamikiwa wa kwanza ambaye amekwenda mbele na kutoa taarifa kwa umma katika gazeti la Daily News la Februari 11, 2023, hivyo hawawezi kusubiri kuona kitu gani kilichowaaminisha walalamikiwa kwenda kinyume cha hukumu ya Baraza.

Alisema kama hivyo ndiyo ilivyokuwa kutokana na hali hiyo hawataenda mbali zaidi kutengeneza uamuzi wao kwa kuhofia kuingia katika shauri la msingi.

"Kwa hiyo tunaona hilo tukio la kuunganisha kampuni lisimamishwe katika hatua hiyo, ili wapate nafasi katika maombi ya msingi mbele ya wadaawa wote tuone kama maombi haya mapya yalikuwa sahihi kuwapo au maombi ya mapitio yangefaa zaidi," ilisema sehemu ya madai.

Jaji Maghimbi alisema kwa ujumla, mbele ya Baraza kuna madai kwamba hukumu ya Baraza imedharauliwa na kutoheshimiwa na walalamikiwa hivyo kuwepo na madai ya kutoheshimu Baraza matokeo ambayo yanaweza kuwa mabaya kwa walalamikiwa.

"Hata hivyo kwa kuwa sheria inasisitiza pande zote mbili zisikilizwe na Baraza katika madai haya, tunaona kwamba kama vitendo vyao vimesababisha kuidharau Baraza au la, tutaangalia mpaka hapo pande mbili zitakapopewa nafasi ya kusikilizwa.

"Taarifa mpya ya kuzuiwa kuunganishwa kwa kampuni hizo na madai ya kudharau amri ya Baraza ni madai yanayohitaji Baraza hili kuwa makini. Mwisho tunaona umuhimu wa kutolewe amri za muda hadi Baraza litakapojiridhisha .

"Uunganishaji wa kampuni kati ya Scancem International DA na Kampuni ya saruji ya Tanga kama ilivyotangazwa na Tume ya Ushindani katika Gazeti la Daily News unasimamishwa hadi maombi yatakaposikilizwa pande mbili," alisema Mwenyekiti.

Alisema Baraza la Ushindani limezuia BRELA na Soko la Hisa Dar es Salaam kuendelea na hatua yoyote ya kuhamisha hisa kutoka Kampuni ya Saruji Tanga kwenda kwenda Scancem International DA.

## Ziara ya Samia yaleta neema kwenye mifugo

**Na Mbaraka Kambona**

ZIARA ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan aliyoifanya Oktoba, mwaka jana nchini Qatar, imeendelea kuvuta wawekezaji kutaka kuwekeza kwenye sekta ya mifugo nchini.

Hayo yalifahamika baada ya Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Widam Food, Al Noubay Al Marri, wa Qatar kumtembelea Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega jijini Dodoma juzi.

Akizungumza katika kikao baina yake na Waziri Ulega, mkurugenzi huyo alisema uamuzi wa kutaka kuwekeza hapa nchini ulipata msukumo kufuatia ziara ya Rais Samia aliyoifanya nchini Qatar.

Alisema lengo la ziara yake ni kukamilisha hatua za kuanzisha kampuni ya Widam Food nchini ambayo inashughulika na biashara ya nyama.

"Tunamshukuru Rais Samia kwa kutufungulia milango ya uwekezaji hapa Tanzania na sisi tunaona nyama ya Tanzania ina mustakabali mzuri kibiashara nchini Qatar," alisema Al Noubay.

Waziri Ulega alisema serikali imedhamiria kuboresha uzalishaji wa sekta ya mifugo, hivyo ujio wa mkurugenzi huyo unaunga mkono jitihada za serikali.

"Sisi tunawakaribisha hapa Tanzania, Rais Samia ameshafungua njia. Kilichobaki ni sisi kuwawezesha ninyi ili uwekezaji wenu ufanikiwe,"alisema Ulega.

Aidha, alitumia fursa hiyo pia kumwahidi ushirikiano mkurugenzi huyo huku akimweleza kuwa akihisi kupata changamoto yoyote asisite kuijulisha wizara, ili itatuliwe.

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe.

HABARI KITAIFA

# Ole Sabaya ahukumiwa kifungo nje mwaka mmoja na masharti

**Na Mary Mosha** MOSHI

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi ya Moshi mkoani Kilimanjaro, imemhukumu kifungo cha nje cha mwaka mmoja aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, baada ya kukiri kosa kwa utaratibu wa 'plea bargaining' katika kesi namba 32 ya mwaka 2023.

Makosa hayo ni kuvamia madaraka yasiyo yake na kula njama na kuzuia haki kutendeka baada ya kufanya upekuzi kwa mfanyabiashara mmoja aliyeko Hai mkoani Kilimanjaro.

Sabaya alibakia kwenye kesi namba 2 ya mwaka 2022 baada ya wenzake Sylvester Nyegu, Nathan Msuya, John Aweyo na Antero Asey ambao waliachiwa Septemba 7 mwaka 2022 baada ya kufanya 'plea bargaining' na Mwendesha Mashatka wa Serikali.

Tangu kesi hiyo kuanza kwake haikuwahi kusikilizwa kutokana na sababu mbalimbali za kisheria, ikiwamo mahakama kukosa uwezo wa kusikiliza, hakimu kuwa na kazi nyingine nje ya kituo chake cha kazi na kutokamilika kwa upelelezi.

Kesi hiyo iliyofunguliwa na DPP ilisikilizwa na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salome Mshasha, ambayo jana ilikuwa kuweka nyaraka pamoja na kusomewa maelezo ya awali.

Lakini upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili Mwandamizi wa Serikali, Verediana Mlenza akisaidiwa na Sabitina Mcharo, ulidai kuwa wamepokea barua kutoka kwa mshtakiwa akiomba makubaliano nje ya mahakama na DPP.Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa mshtakiwa huyo alifanya upekuzi kwa mfanyabiashara mmoja wilayani Hai.



Akisomewa maelezo ya kosa, alidai Januari 19 hadi Machi 30, 2021 kwa nyakati tofauti, Sabaya na wenzake (hawakuwapo mahakamani) katika maeneo ya Kilimanjaro na Arusha, alitumia mamlaka yake vibaya akiwa Mkuu wa Wilaya kumvamia mfanyabiashara, Alex Swai.

Alidai alichukua zaidi ya Sh. milioni 15, kishikwambi, saa na mkufu wa dhahabu na kuagiza mkewe (Gema Maro), Oldasipha Massawe (Mama wa Alex) na Upendo Swai (Dada wa Massawe) kuwekwa katika kituo cha polisi Bomang'ombe.

"January 23, 2021, Sabaya alidaiwa kuagiza Godbless Swai (Kaka wa Swai) apelekwe kwenye nyumba ya mkuu wa wilaya na kumtaka atoe Sh. milioni 50 ili kumsaidia nduguye Alex Swai asipelekwemahakamani kwa kosa la kukwepa kodi huku wenzake wakijifanya maofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Usalama wa Taifa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kwamba fedha hizo zililipwa kwa awamu tatu.

Ilidaiwa kuwa fedha hizo zililipwa Januari 23, Februari 3 na 9 na kwamba Februari 24,2021, familia hiyo iliachiwa na kurejea nyumbani na kisha kuripoti TAKUKURU.

Upande wa utetezi ukiongozwa na Moses Mahuna, Helena Mahuna na Faudhia Mustapher, uliomba mahakama hiyo kumwonea huruma mteja wao na kuongeza kuwa ni kosa lake na kwanza na wazazi mtoto wanamtegemea.

Akitoa hukumu, Mshasha alisema mahakama kwa kuzingatia maelezo ya pande zote mbili, imemtia hatiani chini ya kifungu namba 38 cha Sheria ya Makosa ya Adhabu kifungo cha nje cha mwaka mmoja, bila kukutwa na kosa lolote la jinai.

"Umehukumiwa kifungo cha mwaka mmoja nje bila kufanya makosa yoyote ya kijinai. Unaweza kukata rufaa (rufani) kama haujaridhika na adhabu, ingawa sitegemei kuwa utatenda kosa ikizingatiwa kuwa umekaa muda mrefu gerezani,"alisema.

Sabaya amesota magereza kwa siku takribani 660 bila dhamana akikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi na utatatishaji wa fedha.

# Vyama sita vyalamba bilioni 17/- ruzuku

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema mwaka wa fedha 2022/23 serikali ilitoa ruzuku ya Sh. bilioni 17.5 kwa vyama vya siasa sita kwa lengo la kuimarisha demokrasia.

Amevitaja vyama hivyo ni NCCR-Mageuzi, CCM, CHADEMA, DP, CUF na ACT-Wazalendo.

Majaliwa aliyasema hayo jana bungeni Dodoma wakati akiwasilisha Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2023/24 huku akiomba kuidhinishiwa Sh. 173,733,110,000.

Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu, imeomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. 165, 627,897,000 kwa ajili ya Mfuko wa Bunge.

Waziri Mkuu Majaliwa, aliwaomba viongozi wa vyama vya siasa kuhamasisha wanachama na Watanzania wenye sifa za kujiandikisha kwenye daftari hilo, kupata kitambulisho halali cha mpiga kura pale zoezi hilo litakapoanza rasmi.

"Katika mwaka 2022/23, serikali imetoa ruzuku Sh. bilioni 17.5 kwa vyama vya siasa sita vyenye sifa ya kupata ruzuku. Hatua hii, imesaidia kuendeleza na kuimarisha uendeshaji wa shughuli za vyama vya siasa na demokrasia nchini.

Akizungumza na Nipashe kwa simu, Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itifaki na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alikiri kwamba ni kweli chama hicho kimeanza kupokea ruzuku Machi, mwaka huu.

"Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa (Tundu Lissu), alishasema tumeanza kupokea ruzuku Machi, mwaka huu, na hiyo si siri. Makamu Mwenyekiti alishatoa hiyo kauli na ni kauli sahihi. Walichosema kwamba ni haki yetu tunastahili kupata ni Sh. milioni 107 kwa mwezi," alisema Mrema

Naibu Katibu Mkuu-Bara, NCCR Mageuzi, Anthony Komu, alisema chama hicho kinapokea kwa mwezi Sh. 8,532,000 kwa miezi 27.

"Ni kweli tunapokea ruzuku lakini ruzuku yetu ni kama Sh. 316,000 kwa mwezi. Tulianza kupokea ruzuku hiyo Desemba 2020 mpaka leo ni miezi 27." alisema Komu.

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi-CUF (Bara), Magdalena Sakaya, alisema wanalipwa ruzuku lakini haizidi Sh. milioni nane kwa mwezi.

"Ni kweli CUF inapokea ruzuku kuendana na idadi ya wabunge ilionao bungeni, ambao ni watatu, mmoja kutoka Bara na wawili kutoka Zanzibar. Hiyo ruzuku haifiki milioni 10 iko chini ya milioni nane kwa mwezi," alisema Sakaya

Kadhalika, Katibu Mkuu wa ACT Wazalendo, Ado Shaibu, alisema chama chao kinapokea ruzuku ya Sh. milioni 10 kwa mwezi.

UCHAGUZI MKUU

Majaliwa alisema mwaka wa fedha 2023/24, serikali itaandaa kanuni za uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani, kufanya maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, kulifanyia maboresho daftari la kudumu la wapiga kura na uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika mwaka ujao.

"Katika mwaka 2023/2024, shughuli za maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 pamoja na uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika mwaka 2024 zitaendelea. Kazi zitakazofanyika ni kulifanyia maboresho daftari la kudumu la wapigakura," alisema na kuongeza:

"Kuboresha mifumo ya menejimenti ya uchaguzi, kuendelea na mchakato wa marekebisho ya sheria za uchaguzi; kuandaa kanuni za uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani; na kutoa elimu ya mpiga kura kwa wananchi." alisema Waziri Mkuu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Dk. Joseph Mhagama, akiwasilisha taarifa kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera na Uratibu kwa mwaka wa fedha 2022/23 pamoja na maoni ya kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24, alisema ofisi hiyo inaomba kuidhinishiwa Sh. 9,188,506,000 kwa ajili ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

Kati ya fedha hizo, Sh. 5,079,946,000 ni fedha za ndani na Sh. 4,108,560,000 ni fedha za nje.

Katika maoni ya jumla, Dk. Mhagama, alisema kamati yake inasisitiza serikali iweke malengo ya ukusanyaji maduhuli ambayo yanaakisi uwezo wa ukusanyaji na hali halisi ya vyazo vya mapato.


Form 281d

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

Advertisement of Winding-up Petition
Pursuant to section 281 of the Companies Act 2002

IN THE MATTER OF: KEEN FEEDERS LIMITED COMPANY

A Petition to wind up the above-named Company, of:

Address: P.O. BOX 13365 ARUSHA
TANZANIA

presented on: 19 JULY 2022

by: (name and address of petitioner) JACKLINE MICHAEL MASSAWE
P.O. BOX 2531
ARUSHA- TANZANIA

claiming to be a creditor of the Company,

will be heard at: (Name of Court) HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
SUB-REGISTRY OF ARUSHA

on (date): 29 MAY 2023

at (time): 11:00 AM

(or as soon thereafter as the petition can be heard)

Any person intending to appear on the hearing of the Petition (whether to support it or to oppose it) must give notice of his intention to do so to the petitioner or his / its Advocate in accordance with Rule 3.16 of the Companies (Insolvency Rules) 2003 by 16:00 hours on the business day before the date of the hearing given above.

The Petitioner's Advocate is: ALLEN GODIAN
HAKIKA LAW PARTNERS.
P.O.BOX 2531 ARUSHA.

ALLEN GODIAN Advocate Notary Public & Commissioner For Oaths P.O.BOX 2531, ARUSHA

Dated 04th April 2023

HABARI KITAIFA

# Uwajibikaji kwa viongozi, hukumu ya kifo vyaibuka tume hakijinai

**Na Restuta James**

WAZIRI Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais Mstaafu, Jaji Joseph Warioba, ametaja mambo matano ambayo ni uzalendo, uadilifu, uaminifu, weledi na uwajibikaji kwamba yanapaswa kuzingatiwa katika ngazi zote ili kuleta ustawi, ikiwamo mifumo ya hakijinai.

Aidha, amependekeza kuwa viongozi wakubali kujiuzulu pale sekta wanazozisimamia zinapokumbwa na kashfa kama sehemu ya uwajibikaji.

Jaji Warioba alitoa mapendekezo hayo matano ambayo yanafanana na tunu zilizokuwa zimewekwa kwenye Rasimu ya Katiba, jijini Dar es Salaam jana mbele ya Tume ya Kurekebisha Mifumo ya Hakijiani, inayoongozwa na Jaji Mkuu Mstaafu, Mohamed Othman Chande.

Alisema taasisi zinazoshughulikia mifumo ya haki zimekuwa zikiingiliwa na kupewa maelekezo na wanasiasa licha ya kwamba zinaendeshwa kwa misingi ya sheria, kanuni na taratibu.

Kwa mujibu wa Warioba, anatarajia kwamba mapendekezo yatakayotokana na Tume ya Jaji Chande yatasaidia mifumo ya hakijinai kufanya kazi zake kwa uzalendo, uadilifu, uaminifu, weledi, bidii na kwa nidhamu.

"Lakini ili hiyo iwezekane, ni lazima tuone vyombo hivi vijulikane vinafanya katika mazingira gani, vinafanya kazi katika jamii, je, jamii hii ina uzalendo wa kutosha? Ina uadilifu wa kutosha? Ina uaminifu wa kutosha? Kuna weledi? Wanafanya kazi kwa bidii na nidhamu? Nikasema bado hata kwenye jamii kuna upungufu huu. Pamoja na kutaka hivi vyombo viweze kufanyakazi vizuri, basi jamii nayo ni lazima ibadilike," alisema.

Jaji Warioba ambaye pia amewahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika uongozi wa Awamu ya Kwanza, alisema: "Dosari tulizo nazo ziko mahali pengi katika taasisi zetu nyingi. Ungeweza kusema kwa upande wa wanasheria kuna matatizo ya aina hiyo hiyo, kwa upande wa wana habarikuna matatizo hayo hayo, wahasibu, wahandisi, kwa hiyo ni lazima jamii nayo tujitazame tujaribu kubadilika," alisisitiza.

Alipendekeza kuwa viongozi watumie nafasi zao kusaidia taasisi za hakijinai kutimiza majukumu yake badala ya kuzitumia kwa maslahi binafsi kwa kuzipa maelekezo yaliyo kinyume na mifumo yake ya utendaji.

"Viongozi wasaidie vyombo hivi vinaendeshwa kwa sheria, kanuni na taratibu; vina mifumo yao. Wasije wakaingilia vyombo hivi katika kufanya kazi yake. Vifanye kazi kama sheria inavyoelekeza kwa sababu wakati mwingine wamepewa maagizo ambayo naona hayamo katika mfumo wa ufanyaji kazi," alisema.

Warioba alisema katika miaka ya karibuni, kamati za ulinzi na usalama zimekuwa zikitoa maelekezo kwa taasisi hizo hususani Jeshi la Polisi, ambayo yapo kinyume na utendaji wa jeshi hilo.

Alisema maelekezo hayo yanaweza kutafsiriwa vibaya hivyo ni muhimu viongozi waviachie uhuru wa kiutendaji ili viweze kutimiza majukumu yake kwa weledi.

Kamati za Ulinzi na Usalama zipo katika ngazi zote za utendaji na Mwenyekiti wa vikao ni Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Wenyeviti wa serikali za mitaa; ambao wanatokana na vyama vya siasa.

"Na nimezungumzia kuhusu mfumo wa baadhi ya vyombo. Nikasema TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa), haikukusudiwa kuwa jeshi kwa sababu tayari tuna jeshi la polisi, kilikuwa chombo cha kusaidia kuzuia rushwa kifanyekazi zaidi kwa kuzuia rushwa sio kazi ya kipolisi. Na ni chombo kilichokuwa kinatakiwa kiwe huru kufanyakazi zake bila kupata maelekezo kutoka kwa viongozi," alisisitiza.

Alisema badala ya kufanya kazi hiyo, TAKUKURU imekuwa ikifanyakazi ya kukamata watu huku ikipokea maelekezo kutoka kwa viongozi wa juu.

Jaji Warioba ambaye pia alikuwa Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, alisema taasisi hiyo inapaswa kufanyakazi yake kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

"Unakuta sasa hivi viongozi wengi sana wanatoa maelekezo kwa TAKUKURU na ni maelekezo yanayohusiana na kazi za kipolisi. Mimi mawazo yangu ni kwamba tuijenge TAKUKURU kama ilivyokusudiwa sio kuwa chombo cha viongozi," alisema Jaji Warioba.

Kuhusu Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (DPP), Jaji Warioba alisema inatakiwa kufanyakazi kwa ushirikiano na Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwa huru kutoa ushauri muafaka kabla ya kupeleka kesi mahakamani ama vinginevyo.

**VIONGOZI KUWAJIBIKA**

Kuhusu viongozi kuwajibika, Jaji Warioba alisema viongozi wanapaswa kujua na wao ni sehemu ya matatizo pindi sekta zao zinapokumbwa na kashfa na kuwataka wakubali kuwajibika.

"Na wenyewe wana wajibu maana wakati wote tunasema yanatokea hapa watendaji wanamwangusha rais, lakini wao ni viongozi, wakubali kuwajibika kama kumetokea tatizo mahali, kuna kiongozi pale, na yule kiongozi ndiye anatakiwa ahakikishe kwamba pale mambo yanawekwa sawa, yakiwa mabaya na yeye awajibike," alisema.


COOKFUND
clean cooking solutions

Mradi wa Kuongeza Upatikanaji na Utumiaji wa Nishati Safi na Vifaa Bora vya Kupikia Nchini Tanzania

**WITO WA PILI WA ANDIKO LA KUOMBA UFADHILI**

**Muhtasari**

Programu ya CookFund, inayofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (European Union), ni programu ya miaka mitatu (2022 - 2024) inayolenga kuharakisha upatikanaji wa nishati safi na vifaa bora vya kupikia Tanzania Bara, ikilenga mikoa mitano ambayo ni **Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma na Mwanza**. Programu hii inatekelezwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Mitaji (UNCDF) kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO) na Wizara ya Nishati nchini Tanzania.

Programu hii inatoa msaada wa kifedha na kiufundi kwa madhumuni ya kuchangia juhudi za Tanzania katika mapambano dhidi ya mabadiliko ya hali ya hewa kwa kuongeza idadi ya watu wanaotumia nishati bora na endelevu za kupikia, na hatimaye kuboresha mazingira, ajira na fursa za kibiashara. CookFund inatoa msaada kutokana na matokeo yatakayofikiwa (performance based), kwa madhumuni ya kutatua changamoto za mitaji kwa wafanyabiashara na pia kutoa unafuu wa bei kwa watumiaji wa mwisho wa nishati zinazolengwa (gesi ya kupikia, majiko sanifu ya mkaa, majiko ya umeme ya mvuke, *bioethanol* na mkaa mbadala).

**Wito wa Maandiko ya Kuomba Ufadhili**

UNCDF inawakaribisha wafanyabiashara na makampuni yanayojishughulisha na mnyororo wa thamani wa nishati safi na vifaa/teknolojia bora za kupikia katika maeneo ya mijini ya mikoa ya mradi, kuandika na kuomba ufadhili wa kiufundi na kifedha kupitia wito huu wa pili katika Programu ya CookFund.

**Maombi:** Mwongozo, Vigezo na Fomu maalumu ya maombi, zinaweza kupakuliwa kutoka kwenye tovuti ya mradi, i.e. *https://www.uncdf.org/cookfund*.

**Lugha:** Maombi yote yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.

**Mwisho wa kuwasilisha maombi:** Raundi ya pili ya maombi itakuwa wazi kuanzia tarehe 6 April 2023 mpaka tarehe 30 September 2023.

**Warsha kabla ya uwasilishaji:** UNCDF itaandaa warsha ya siku moja ili kutoa fursa kwa waombaji (watakaopenda) kupata maelezo zaidi juu ya mwongozo wa maombi na kutoa fursa kwa waombaji kuuliza maswali. Ikiwa unataka kushiriki warsha hii, tafadhali tuma barua pepe kwa *cookfund.tz@uncdf.org* yenye kichwa cha habari *"Warsha ya CookFund"*. Tafadhali onyesha mkoa unakofanyia kazi zako (*yaani, Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Dodoma na Mwanza*). Tarehe na ukumbi wa warsha vitathibitishwa kwa washiriki. Waombaji watatakiwa kubeba gharama zao wenyewe za kuhudhuria warsha hii.

*Agalizo: Kuhudhuria katika warsha hii sio sehemu ya masharti/vigezo vya kutuma maombi ya ufadhili.*

Kwa taarifa zaidi au maswali, tafadhali wasiliana na:
UNCDF Tanzania, Barua pepe: *cookfund.tz@uncdf.org*
Tel: +255 22 260 0911

MINISTRY OF ENERGY — UNCDF Impact Capital for Development — UNIDO — Funded by the European Union


## Biteko awakingia kifua wachimbaji wadogo

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Madini, Dk. Doto Biteko, ameagiza taasisi mbalimbali za serikali kuwasaidia wachimbaji wadogo wa madini kuliko kutumia muda mwingi kuwawinda, kuwasaka na kuwatengenezea hesabu hewa.

Biteko pia ameagiza wenye viwanda kuhakikisha wananunua madini kwa bei elekezi badala ya kuwanyonya wachimbaji wa madini. Waziri Biteko aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa wachimbaji wadogo na wadau wa madini ya viwandani wenye kaulimbiu 'Madini ya Viwandani kwa Uchumi na Mazingira Bora'.

"Wanatumia muda mwingi kuwasaka kila mahali na kuwatengenezea mahesabu ambayo hata hayapo ndiyo maana tumekubaliana na Wizara ya Fedha na Mipango tunapita kwa wachimbaji wetu tunapojadili masuala ya kikodi tuwashirikishe kuanzia mwanzoni haina maana ya kuja na kodi bila kuwashirikisha halafu kesho utarajie watalipa kwa furaha," alisema Biteko.

Alisema Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Tume ya Madini waende kwa wachimbaji na kuwajulisha mipango ya kikodi watalipa kwa furaha na mapato yataongezeka.

Waziri Biteko alisema Rais Samia hataki kuona misukosuko anataka kila mmoja awe na furaha katika hii nchi kwa sababu wote ni Watanzania.

Aidha, alisema sekta ya madini imekuwa kwa kiwango kikubwa asilimia 80 ya mapato yanayotokana na sekta ya madini kwenye zao moja la dhahabu.

"Hii dhahabu inachimbwa wapi ni maeneo machache. Madini ya viwanda na madini ya ujenzi yanachimbwa kila mahali nchini, lakini mchango wake bado ni mdogo hii ni kwa sababu hatujasimamia vya kutosha,"alisema Biteko.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan mchango wa sekta ya madini viwandani umeongezeka kwa kiwango kikubwa kutoka Sh. milioni 451.6 hadi Sh trilioni 1.19, Februari mwaka huu.

Aidha, aliwataka wachimbaji wa madini kuhakikisha wanapeleka madini yenye ubora "Ninazo taarifa wapo wachimbaji wengine wanavyochimba madini mengine wanachanganya na vitu vingine ili kuongeza uzito,"alisema.

Biteko alisema kitendo hicho ni kusababisha hasara kwa wenye viwanda na hatimaye watafilisika na kuamua kuondoka na kujikuta wanakosa soko la kuuza madini yao.

Alisema hakuna mtu ambaye anaweza kuagiza malighafi nje ya nchi kama zinapatikana nchini kwa ubora unaotakiwa na kwa bei nafuu.

"Wakati wanawalalamikia wenye viwanda kuwapunja na ninyi wachimbaji uzeni malighafi zikiwa katika ubora unaotakiwa,"alisema Waziri Biteko.

Alisema sera ya madini inaelekeza, madini yote ambayo yanachimbwa nchini walau kwa kiwango kikubwa yaongezewa thamani kwa kuwa asilimia kubwa ya madini hayo hutumika katika viwanda na ujenzi.

Aidha, aliwaomba wenye viwanda na wachimbaji madini kuendelea kupeana ushirikiano, ili waweze kukuza sekta hiyo.

Alisema Wizara inatambua changamoto zilizopo katika uchimbaji wa madini ya viwanda hasa ukosefu wa mitaji , ukosefu wa taarifa za deolojia, ubora wa madini yanayohitajika kwa ajili ya viwanda, uwepo wa wasambazaji wa madini wasiokuwa na leseni na kutokununuliwa madini kwa bei elekezi.

TANGAZO

KCB BANK

# Tariff Guide

| SERVICE | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | TZS | USD/EURO | KES | GBP |
| **STATEMENTS** | | | | |
| Monthly Statement | free | free | free | free |
| Duplicated Statements per page (excluding community account) | 2,000 per page/Free via email | 1.30pp | 78pp | 0.70pp |
| Interim Statement per page (excluding community account) | 2,000 per page/Free via email | 1.30pp | 78pp | 0.70pp |
| Balance Enquiry | 1,500 | equivalent | equivalent | equivalent |
| **ATM VISA DEBIT CARD** | | | | |
| ATM Card Issuance (for the first time) | 7,500.00 | 5 | n/a | n/a |
| ATM withdrawal from KCB ATMs (per transaction) | 1,000.00 | equivalent | n/a | n/a |
| ATM withdrawal from Non-KCB ATMs (Tanzania) | 2500 | 1.3 | n/a | n/a |
| ATM withdrawal from Non-KCB ATMs (International) | 6500 per each 400,000 limit | 3.3 | n/a | n/a |
| ATM mini statements | free | free | n/a | n/a |
| Daily Limit | 2,000,000.00 | equivalent | 50000 | equivalent |
| POS and E-commerce daily limit | 5,000,000.00 | 2,500 | n/a | n/a |
| Minimum withdrawals | 5000 | equivalent | n/a | n/a |
| ATM Card Repalcement (lost/destroyed cards) | 7,500.00 | 5 | n/a | n/a |
| Blocking/unblocking ATM cards | free | free | n/a | n/a |
| Card Renewal | 7,500.00 | 5 | n/a | n/a |
| Quarter maintenance fee | 1,000 | 1 | n/a | n/a |
| Camera viewing | 30,000 | equivalent | n/a | n/a |
| **STANDING ORDER** | | | | |
| within KCB | 2500 | equivalent | equivalent | equivalent |
| Outward to other banks | 5000 | 3 | n/a | n/a |
| Setup/Amend Standing Order | 8,000.00 | 7 | 500 | 4 |
| Unpaid Standing Order (penalty) | 10000 | 10 | 500 | 10 |
| **CHEQUES** | | | | |
| Unpaid Cheque (insufficient funds) - Outward | 15000 | 13 | n/a | n/a |
| Unpaid Cheque (insufficient) - inward | 65000 | 52 | n/a | n/a |
| Unpaid Cheques - technical | 15000 | 15 | n/a | n/a |
| USD unpaid cheque | 52 | 52 | n/a | n/a |
| Counter Leaves | 13000 | equivalent | equivalent | equivalent |
| Bankers Cheque | 30,000.00 | 30 | n/a | n/a |
| Stop payment-per set up | 25000 | 25 | 1300 | 13 |
| New cheque book retail | 600 per leaf | equivalent | equivalent | equivalent |
| **TT's INTERNATIONAL** | | | | |
| Outward | 55USD(equivalent) over the counter /45 USD(equivalent) for IB | 55USD over the counter /45 USD for IB | equivalent | equivalent |
| Inward TT (excluding community accounts) | 13USD (TZS equivalent) | 13USD(Euro equivalent) | equivalent | equivalent |
| Recall of funds/Cancellation of TT | 10USD (TZS equivalent) | 10USD(Euro equivalent) | equivalent | equivalent |
| Intercompany transfers (KCB to KCB Regional Transfers) | 40USD (TZS equivalent) | 40USD(Euro equivalent | equivalent | equivalent |
| Amendment of TT (Customer induced) | 10USD (TZS equivalent) | 10USD(Euro equivalent) | equivalent | equivalent |
| **TRANSFERS LOCAL** | | | | |
| KCB to KCB | 3,000 over the counter/1,500 on IB | equivalent | equivalent | equivalent |
| EFT (KCB Tanzania to any local bank) | 3500 over the counter /1,500 on IB | 3 | n/a | n/a |
| TISS/local TT (excluding community account) | 10000 | 13 | n/a | n/a |
| East African Payments (EAPS) | 10000 | n/a | 870 | n/a |
| **MINIMUM A/C OPENING BALANCE** | | | | |
| Current Account-Company(SME&CORPORATE) | 100000 | 100 | 5000 | 13 |
| Current-Personal | 50000 | 100 | 5000 | 65 |
| Mapato Account | 10000 | 10 | 500 | 10 |
| KCB Junior Account | 10000 | 10 | 500 | 10 |
| KCB Student Account | 10000 | 10 | 500 | 10 |
| KCB Simba Savers | 50000 | 50 | n/a | n/a |
| A/C CLOSURE | | | | |
| Closing account | Free | 39 | 2200 | 26 |
| **OTHER SERVICES** | | | | |
| Search of old documents | 20,000 | 13 | 900 | 10.5 |
| Forex Cash Deposits (smaller denominations below US $ 50) | n/a | 8% for denominations that are less than USD 50 | n/a | 8% for denominations that are less than USD 50 |
| Dormant Account Activation | free | free | free | free |
| **ACCOUNT MAINTAINANCE FEES** | | | | |
| Counter Withdrawals (excluding: Simba,Cub & Community accounts) | <10million 2500 > 10million 0.1% max 20000 | 0.50% | 0.50% | 0.50% |
| Ledger Fees - Current Accounts (excluding community and salary) | personal current account 10,000, business 20,000, corporate account 30,000 | personal current 10USD/Business 16USD/ Corporate 20USD | 700 | personal current 10GBP/Business 16GBP/Corporate 20GBP |
| Ledger Fees - Savings Accounts (Exclude Simba, Cub, Salary & Student Accounts) | Mapato 1,500 | 7 | 176 | 7 |
| **THIRD PARTY ENCASHMENT** | | | | |
| Withdrawal fee to be paid by the beneficiary | 6500/13USD | 13 | 13 | 7 |
| Annual setup fee (SME's and Corporate) to be paid in by the account holder | 50,000 | 50 | 4400 | 33 |
| **SALARY PROCESSING** | | | | |
| Salary processing | 4,000 over the counter / 3,000 IB | equivalent | 130 | equivalent |
| **CERTIFICATE OF BALANCE** | | | | |
| Balance of Account (Flat fee per certificate) | 39000 | equivalent | equivalent | equivalent |
| Auditors Confirmation (flat per certificate) | 30000 | equivalent | equivalent | equivalent |
| Reference Letters | 30000 | equivalent | equivalent | equivalent |




| TRADE FINANCE | |
|---|---|
| | |
| **IMPORT LETTER OF CREDIT** | |
| LC ISSUANCE/extension/increase amount | 1.3% Per Quarter |
| Normal Amendment | 130 USD |
| Release Commision/lc document processing | 20 USD |
| RETIREMENT | 0.30% minimum 100 maximum 200 |
| CANCELATION | 260 USD |
| **EXPORT LETTER OF CREDIT** | |
| ADVISING | 200 USD |
| NEGOTIATION | 0.60% min 200 max 300 |
| DISCOUNTING | 0.80% |
| AVALIZATION | 0.80% |
| **DOCUMENTS FOR COLLECTION** | |
| Documents HANDLING FEE | 150 USD |
| COURIER | 150 USD |
| **GUARANTEE** | |
| Issuance fee | 1.30% |
| AMENDMENT/Reduce of amount | 130 USD |
| DISCREPANCY | 55 USD |
| EXAMINATION | |
| **OTHERS** | |
| SWIFT | 50 USD |
| Tracer | 50 USD |
| COURIER | 150 USD |
| | |
| **MOBILE BANKING CHARGES** | |
| Balance enquiry | free |
| Mini statement | 300 |
| Invite Friend | free |
| Cheque book | 300 |
| Stop cheque | 300 |
| Stop card | 300 |
| Change Pin | free |
| Full statement | 500 |
| | |
| **BILL PAYMENTS** | |
| TANESCO(LUKU) | 1.1% of the transacted amount |
| DAWASCO | 1300 |
| DSTV | Free |
| STARTIMES | Free |
| ZUKU | Free |
| SMILE | Free |
| UHURU | Free |
| AZAM | Free |
| SASATEL | Free |
| **SEND MONEY TO E-WALLET** | |
| Mpesa<br>Airtel Money<br>Tigo Pesa<br>Eazzy Pesa | 1000 to 100000 - 1000, 100001 to 200000 - 1500, 200001 to 400000 - 2000, 400001 to 600,000 - 3000, 600001 to 800000-5500, 800001 to 1000000 - 7000, 1000001 to 2000000 - 10000, 2000001 to 3000000 - 15000. |
| **FUNDS TRANSFER** | |
| Own accounts | Free |
| KCB accounts | 1000 |
| **IB TRANSACTION CHARGES** | |
| M Pesa<br>Airtel Money<br>Tigo Pesa | 5000-50000-1000, 50,0001 to 100,000 - 1500, 100,001 to 200,000-2,500,200,001 to 400,000 - 3,000, 400,001 to 600,000 -3,500, 600,0001 to 800,000 - 4,000, 800,001 to 1,000,000 - 5,000, 1,000,001 to 1,500,00 - 7,500,1,500,001 to 2,000,000 -10,000, 2,000,001 to 2,500,000 - 12,500,2,500,001 to 5,000,000 - 15,000. |
| **INTERCOMPANY TRANSACTION CHARGES** | |
| Inter-company cash withdrawals charges | 0 up to 60 USD charge 4 USD |
| | 60.01 up to 250 USD charge 7.50 USD |
| | 250.01 up to 1,250 USD charge 13 USD |
| | 1,250.01 up to 6,250 USD charge 26 USD |
| | Above 6,250 USD charge 1.20% of daily cumulative withdrawals |
| Inter-company cash deposit charges | 0 up to 250 USD charge 3USD |
| | Between 250.01-1250 USD charge 7USD |
| | Between 1250.01- 6250 USD charge 13 USD |
| | Above 6250 USD charge 0.60% of daily cumulative deposits |
| Intercompany standing orders across all companies | Intercompany standing order 13 USD |
| | |
| **LOANS** | |
| Processing/arrangement/appraisal fees | |
| Asset finance | 2.40% |
| Business loans: | 2.40% |
| Overdrafts: | 2.40% |
| | 2.40% |
| | 2.40% |
| | |
| Penalty on unpaid loan instalment: | 10% above approved rate |
| Early repayment: | NA |
| Valuation fees: | As per service provider rates |
| Legal fees: | As per service provider rates |
| Loan insurance fees: | 1% |
| Interest rates | + or - Base Lending Rate |
| Personal loans: | 19% |
| Business loans: | '+ or - Base Lending Rate |
| | |
| | |
| *Base Lending Rate | 19% for TZS and 9% for USD |
| *All rates are subject to negotitiation based on the product | |
| | |

**NB;**

**1. All staff account will be charged when transacting over the counter and charges excluded on all digital platform**

**2. Community account will be charged on salary processing over the counter and charges excluded on internet banking**

Please note: All taxes included

| Name/Tittle | Signature | Date |
|---|---|---|
| Lulu Shikonyi - Head of Operations | Signed | 05.04.2023 |
| Juma Abdul - Head of Retail Banking | Signed | 05.04.2023 |

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Mtindo wa kuvutana maofisa na wachimbaji ufikie tamati

**KWA** muda mrefu kumekuwa na malalamiko ya wachimbaji wadogo wa madini kuwa katika mvutano na mamlaka za kiserikali kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na taasisi zilizopewa dhamana ya kusimamia sekta hiyo, zikiwamo ofisi za madini za kanda na Tume ya Madini.

Miongoni mwa malalamiko hayo ni kwamba taasisi hizo zimekuwa zikiwadai kodi kubwa ambazo hazina uhalisia hasa kutoka TRA. Wamekuwa wakidai kuwa kodi hizo wanazodaiwa ni kubwa kulinganisha hata na fedha wanazozipata kutokana na shughuli hiyo.

Pia wamekuwa wakidai kubughudhiwa na maofisa madini ikiwamo kunyimwa leseni pindi wanapoomba ili wafanye shughuli zao kihalali. Aidha, madai mengine ya wachimbaji hao wadogo ni kufukuzwa kwenye maeneo ya uchimbaji na maofisa madini wa maeneo husika baada ya kubainika kuwa eneo walilomo lina madini hatua ambayo baadhi ya maofisa madini huingiwa tamaa kwa ajili ya kutaka kuwapatia wachimbaji wakubwa.

Hatimaye kilio hicho, kinaonekana kusikika serikalini baada ya Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko, kuagiza taasisi mbalimbali za serikali kuwasaidia wachimbaji wadogo wa madini kuliko kutumia muda mwingi kuwawinda, kuwasaka na kuwatengenezea hesabu hewa.

Wakati wa ufunguzi wa mkutano wa wachimbaji wadogo na wadau wa madini jijini Dar es Salaam jana, Waziri Biteko alisema TRA mathalan, wanatumia muda mwingi kuwasaka kila mahali na kuwatengenezea hesabu ambazo hata hazipo wala hazina uhalisia wowote.

Kutokana na hali hiyo, Waziri Biteko alisema wizara yake imekubaliana na Wizara ya Fedha na Mipango kupita kwa wachimbaji wanapojadili masuala ya kikodi ili wawashirikishe kuanzia mwanzoni kwa kuwa hakuna maana ya kuwapo kodi ambazo wahusika hawajashirikishwa. Hatua nyingine aliyoitaja ni TRA na tume ya madini kwenda kwa wachimbaji na kuwajulisha mipango ya kikodi, hatua ambayo itawafanya walipe kwa furaha na hatimaye kuwezesha kuongezeka kwa mapato ya serikali.

Hatua ya Waziri Biteko na wizara yake kuliona tatizo hilo ni jambo la kupongezwa kwa kuwa sasa wachimbaji wadogo wanaona ni wakati mwafaka wa wao kulindwa na serikali ili kufanya shughuli zao bila bughudha.

Pamoja na hayo, wakati umefika sasa wa taasisi zilizopewa dhamana katika sekta mbalimbali kama vile madini na TRA, kubadilika na kuwaona wachimbaji na wafanyabiashara wengine ni washirika katika kutimiza azma ya serikali ikiwamo ya kuongeza pato la taifa. Ni jambo la fedheha kuona taasisi inayopewa dhamana kama ya kukusanya mapato ya serikali au kukuza sekta ya madini ikipambana na wadau muhimu katika kutimiza azma iliyokusudiwa.

Hiyo iko wazi kwa sababu kwa miaka kadhaa iliyopita, jamii ilishuhudia wafanyabiashara wadogo na wa kati wakibughudhiwa na maofisa wa TRA kwa madai ya kukusanya kodi. Mbaya zaidi, maofisa hao walikuwa wakiambatana na askari waliokuwa na mitutu kama vile wanawawinda watuhumiwa wa mauaji.

Wahenga wanasema yaliyopita si ndwele, tugange yajayo, hivyo huu ni wakati wa kuwapo kwa mazingira rafiki baina ya mamlaka za serikali na wazalishaji katika kuhakikisha uchumi wa nchi unakua.

Kwa mantiki hiyo, wafanyabiashara na wachimbaji wapewe elimu kuhusu kodi na kuwekewa mazingira mazuri ya kufanya shughuli zao badala ya kuendelea kuwa kwenye wasiwasi wa kubughudhiwa na maofisa wa taasisi za serikali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kumruhusu binti yangu 'kadogoo' aolewe, kwangu bado shida sana

Na Pilly Kigome

**KUNA** usemi 'uchungu wa mwana aujuae mzazi.' Hoja yangu inazama zaidi kwa mzazi wa kike kama mimi, akiwa mhusika mkuu moja kwa moja katika uchungu huo. Kwani yeye ndiye amehangaika na kaubeba mzigo wa tumbo na mateso mengine yatokanayo na ujauzito, hadi kumpata mtoto huyo.

Sina maana baba hana uchungu, la hasha! Baba naye ana uchungu wake, kwani hubeba nafasi kubwa ya majukumu, kuhakikisha mtoto huyo anapata stahiki zake muhimu.

Kutokana msingi huo,sioni vyema mtoto huyo ambaye anatakiwa awe katika uangalizi wa mzazi au bado kuwa darasani, tuanze kumbebesha majukumu ambayo mimi naweza ninaueleza ni ukatili kwa mtoto

Mimi naona tubaki na kauli moja inayosema mtoto ni yule kuanzia umri wa siku moja hadi miaka 18. Huyo aliye mtoto tunapaswa kumuepusha na makinzano kuhusu umri sahihi na haki zinazomuhusu mtoto, mwisho wa siku ndiyo muathitrika.

Kwa uhakika tukiwa na msimamo mmoja tukakubaliana tafsiri ya mtoto ni nani, naamini ama migogoro au kukinzana kwa sheria zetu za ndoa zinazotungwa na taasisi za haki za watoto, au taasisi za dini, hazitaleta mikinzano tena, kwakuwa tayari watu wote tutakuwa tumeshakubaliana umri wake sahihi.

Kwa uelewa wangu, sioni sababu ya mtoto kubebeshwa mizigo iliyomzidi kimo, kwa maana ya majukumu mazito yanayomzidi umri. Ni kitu ninachoweza kukifafanu ni ukatili wa kijinsia, kwani tumemuongezea dozi na kumbebesha mzigo mkubwa sana.

Naongea haya baada ya kuona mkinzano iliyopo kwa sheria za ndoa katika ya taasisi za kiimani, zinazosimamia sheria, kuhusu uhalali wa umri sahihi wa mtoto wa kike kuolewa.

Wasimamizi wa haki za watoto wanasimamia umri wa binti kuolewa iwe miaka 18 na kuendelea. Nikisikia hoja ya kutaka mabinti kuolewa, kwa nafsi yangu kama mama inanipa shida.

Ndio maana tunapaswa kurudi katika pointi yangu ya msingi, kukubaliana katika tafsiri ya mtoto ni nani na yupi mtu mzima kwa kigezo cha umri.

Ndoa ni jambo kubwa sana katika maisha ya mwanadamu na inabeba dhana kubwa, ikiwamo malezi na majukumu ya kuangalia familia. Hivyo, tunapomkabidhi hilo binti asiyekomaa kiumri, kibaiolojia, kisaikolojia na hata kifalsafa, tunamuingiza katika wakati mgumu, anakuwa kule asikotakiwa kuwapo.

Kuna dhana imetawala hata katika mila zetu, mtoto endapo akionekana hajaendelea na masomo, basi anapatiwa wadhifa wa ndoa. Imani ni kwamba, akaachwa huru, anaugulia mimba na familia inapata kashfa.

Kuna mahali hapo baadhi ya wanaharakati wa haki za watoto wanawake, wanakuwa wakali katika dai la kisheria, binti kuolewa katika umri miaka miaka 18.

Huwa kila kukicha katika dunia hii ya uwazi na utandawazi tunasikia taarifa za kitaalamu, shida ya mabinti kuingia kwenye uzazi mapema magumu yanayowapata kiafya.

Tunaweza kudhani yanapita, lakini katika uhalisia wapo wazazi na walezi wanalia. Wahusika walionusurika uhai, nao wanataabika kibaiolojia na hata mustakabali wa maisha yao ya baadaye.

Ndio katika tafsiri hiyo, Rais mwanamke nchini analiona hilo hata kufanya uamuzi kitaifa katika kumtetea mama aliyejikwaa kimajukumu.

Nakumbuka mnamo Julai, 2016 Mahakama Kuu ya Tanzania ilihukumu baadhi ya vifungu hivi vya sheria ya ndoa kwamba ni batili, hasa katika kipengele cha umri wa ndoa.

Hukumu hiyo ilitolewa baada ya kesi iliyofunguliwa na mwanaharakati kutoka shirika binafsi linalomtetea mtoto wa kike, akipinga vifungu vya sheria ya ndoa inayomruhusu mtoto wa kike kuolewa akiwa na miaka 14 kwa kibali cha kisheria, pia miaka 15 kwa ridhaa ya wazazi.

# Wahalifu walivyogeuka walinzi Mikumi

**Na Joseph Mwendapole,** MIKUMI

VIJANA waliokuwa wakiongoza kwa vitendo vya ujangili kwenye Hifadhi ya Taifa ya Mikumi mkoani Morogoro, maarufu kama 'Mapanga Shaa Shaa', sasa wamebadilika na kugeuka walinzi wa mbuga hiyo.

Hayo yalibainika mwishoni mwa wiki iliyopita wakati wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari walipotembelea mbuga hiyo iliyoko kilomita 288 kutoka jijini Dar es Salaam.

Wahariri hao walikuwa kwenye mafunzo ya siku tatu yaliyoandaliwa na Chama cha Wanahabari wa Mazingira (JET) yanayofadhiliwa na Internews Earth Journalism Network East Africa.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Chama cha Mikumi Environmental Conservation Development (MECODE), Musa Buhaki, alisema vijana hao walikuwa wakiingia kwenye hifadhi hiyo na kukamata wanyama kwa ajili ya kwenda kuuza kama kitoweo kujikwamua kiuchumi.

Buhaki alisema baadhi ya vijana hao walikuwa wakijeruhiwa na wanyama wakali na wengine kufariki dunia lakini kwa sasa baada ya kupata shughuli za kiuchumi wameachana na ujangili huo.

"Kwa sasa huwezi kukuta kijana anaingia kwenye hifadhi kufanya ujangili kwa sababu wenyewe ndio wamegeuka kuwa walinzi wa hifadhi na kila mwananchi anayeishi pembeni ya hifadhi amegeuka kuwa mlinzi kwa hiyo si rahisi kufanya ujangili kama ilivyokuwa zamani.

"Kwa kweli vijana walikuwa wanaumia sana wengine wadogo sana umri wa watoto wetu walikuwa wanapotea tukaona hili litaendelea mpaka lini tukaanza kuwaita kuwaingiza kwenye shughuli zetu na kuwalipa fedha kidogo kidogo," alisema.

Alisema baada ya kuanza utaratibu huo vijana hao walianza kuambiana kuhusu shughuli hizo na wengi walianza kukubali kuacha ujangili na kufanyakazi halali ya kusafisha mbuga kwa ujira kidogo.

"Tulianza na vijana wachache lakini kadri siku zilivyozidi kwenda walikuwa wanaambiana na sasa tunakwenda na vijana kuanzia 20 na zaidi tunafanya kazi na kuwalipa kidogo kidogo na wote wamekubaliana na kazi hii. Hawaendi tena kufanya ujangili wa wanyama," alisema.

Alisema wamekuwa wakiokota vyuma chakavu wakati mwingine hadi tani moja na kwenda kuviuza na kupata fedha za kutosha kulipa vijana hao Sh 7,000 kila mmoja kwa siku.

Pia alisema kupitia shughuli hizo za usafi wanachama wa kikundi cha MECODE akiwemo yeye wanasomesha watoto wao kwenye vyuo mbalimbali vya elimu ya juu.

Alisema kabla ya kuanza kazi hiyo ya usafi alikuwa akifanya kazi ya uganga wa kienyeji na akifahamika zaidi kama Dk. Kimbunga kwa watu wa maeneo ya Mikumi.

Hifadhi ya Mikumi ambayo inapitiwa na takribani kilomita 50 za barabara inayotoka Dar es Salaam hadi Tunduma imekuwa ikipoteza wastani wa wanyama 700 kila mwaka wanaogongwa na magari.

Hifadhi hiyo inatarajia kuanza kufunga kamera za usalama barabarani ikiwa njia ya kuwadhibiti madereva ambao hawazingatii mwendo wa kilomita 50 kwa saa wanapokatisha kwenye mbuga hiyo.




Meneja wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB) Tawi la Newala, mkoani Mtwara, Alex Minai (kushoto), akikabidhi sehemu ya msaada wa mifuko 100 ya saruji kwa Mbunge wa Newala, Kapteni mstaafu George Mkuchika, mjini Newala, iliyotolewa na benki hiyo kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa ukuta wa Chuo cha Uuguzi Newala. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wizara SMZ yatahadharisha wanaotumia maji ya chemchem

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imetoa tahadhari kuhusu chemchem inayotoa maji kutoka Bahari ya Hindi katika kijiji cha Msuka Mashariki Pemba, yanayodaiwa kuwa yanatibu maradhi mbalimbali.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema baada ya uvumi wa taarifa ya maji hayo wizara ilitumia wataalamu kwenda kuchukua sampuli ili kuyafanyia uchunguzi.

Alisema baada ya uchunguzi huo wa kina, imebainika kuwa maji hayo sio salama kwa matumizi ya binadamu.

Waziri huyo alisema maji hayo yamebainika kuwa yana vimelea vinavyosababisha magonjwa ya kuharisha na yana idadi kubwa ya baktreia wa E.coli wa idadi kubwa kati ya 220 hadi 1,800 kwa kila lita 100.

"Kwa kawaida maji ya kunywa hayatakiwi kuwapo na hata kimelea kimoja cha aina hiyo," alisema Mazrui.

Waziri huyo alisema pia uchunguzi umebainika kuwepo vimelea vinavyosababisha ugonjwa wa kuharisha aina ya coliforms wa zaidi ya 1,800 kwa kila lita 100.

Alisema kwa kawaida vimelea hivyo vinahitajika viwemo kwenye maji ya kunywa, lakini isiwe zaidi ya watatu kwa kila lita moja kwa kila lita 100.

Pia, alisema uchunguzi huo umebaini uwepo wa chloride kwa kiwango kikubwa, ambapo wataalamu wamebaini kiasi cha upimo wa kuanzia 1490 milligram kwa kila lita moja.

"Kiwango kinachokubalika ni kipimo kisichozidi 250 milligram kwa kila lita moja," alisema.

Waziri huyo alisema kiwango cha chumvi kimebainika kwa kiwango cha kupima ukali wa chumvi cha baina ya nukta nane na tatu katika maji hayo ambapo ni zaidi ya kiwango kinachokubalika katika maji ya kunywa.

Alisema maji hayo yamechafuliwa na kinyesi cha viumbe hai pia kuna kiwango kikubwa cha kemikali ambazo sio salama kwa kunywa na kama wananchi wataendelea kuyatumia yanaweza kuathiri afya zao na kusababisha matatizo ya kiafya.

Mazrui alisema miongoni mwa matatizo hayo ni magonjwa ya kuharisha, ikiwemo kipindupindu, kutapika, kupoteza maji mwilini, kupata maumivu makali ya tumbo na kupata vidonda vya tumbo.

Aliwataka wananchi kupuuza taarifa zilizosambaa katika mitandao ya kijamii kwamba maji hayo yanatibu kwa sababu maji hayo hayawezi kutibu ugonjwa wowote na kuwataka kuacha kuyatumia, ili kuepukana na athari.

Waziri huyo alisema uvumi huo umepelekea maji hayo kusambazwa katika maeneo mbalimbali ya Kisiwa cha Pemba na nje ya nchi ambapo hadi Oman, Congo na Mombasa Kenya yameshasambazwa.

Naye Mkemea Mkuu wa Serikali, Dk. Farid Mzee Mpatani, alisema maji hayo hayafai hata kutumiwa na wanyama au umwagiliaji kwa ajili ya kilimo kutokana na sumu iliyokuwemo.

Aliwataka wananchi kuacha kabisa kutumia maji hayo na wale ambaye wameshatumia kwenda katika vituo vya afya kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa kiafya na kupatiwa matibabu.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

## TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LIMITED (TANESCO)

**REQUEST FOR EXPRESSIONS OF INTEREST
FOR CONSULTING SERVICES**

**Country: TANZANIA, UNITED REPUBLIC OF**

**Name of Project: TANZANIA – ZAMBIA TRANSMISSION INTERCONNECTOR PROJECT (TAZA)
PRACTICE AREA: ENERGY AND EXTRACTIVES SPECIFIC PROCUREMENT NOTICE**

**Credit No.: 6293-TZ**

**Project ID No.: P163752**

**Assignment Title: PROVISION OF CONSULTANCY SERVICES FOR SUPPORTING GENDER AND ENVIRONMENT SAFEGUARD ISSUES INCLUDING CAPACITY BUILDING UNDER TANZANIA – ZAMBIA TRANSMISSION INTERCONNECTOR PROJECT (TAZA)**

**Tender No.: PA/001/2022-23/HQ/C/06**

**Borrower Bid Ref.: TZ-TANESCO-294469-CS-QCBS**

**Issue Date: 04th April, 2023**

1. The Government of the United Republic of Tanzania has received financing from the World Bank towards the cost for undertaking the consultancy services to support gender and environment safeguard issues under the Tanzania – Zambia Transmission Interconnector Project (TAZA) and intends to apply part of the proceeds for consulting services under this tender

.

2. The consulting services ("the Services") include: -
   (i) Develop and implement an Environmental and Social Management System (ESMS) for TANESCO;
   (ii) Develop and implement Occupational Health and Safety Management System (OHSMS) for TANESCO;
   (iii) Monitor and supervise implementation of the project's environmental and social risk management instruments;
   (iv) Support the design and implementation of the Grievance Redress Mechanism (GRM) on environmental, social and gender issues;
   (v) Support the implementation of the Gender Based Violence (BGV) Action Plan;
   (vi) Conduct capacity building to TANESCO staff, project stakeholders and ensure adequate public consultations during implementation
   (vii) Provide overall guidance, supervision, and technical support for implementation of TAZA's four-year (4) gender action plan

   The consultancy contract is expected to take twenty-four (24) calendar months from the date of effectiveness of the contract and the estimated level of effort is 87 staff- months as indicated in the Terms of Reference. The detailed Terms of Reference (TOR) for this assignment is available on TANESCO website through link: **https://tanesco.co.tz/index.php/procurement/current-tenders?own=0.**

3. TANESCO now invites eligible consulting firms ("Consultants") to indicate their interest in providing the Services. Interested Consultants should provide information demonstrating that they have the required qualifications and relevant experience to perform the services.

**The shortlisting criteria are:**

(a) Core business and years in business (submit Certificate of Incorporation of the firm and the Company Profile);

(b) Relevant similar experience which should specifically include: -
   (i) At least ten (10) years' experience in management and implementation of gender equality, environmental and social safeguards preferred on linear infrastructure power projects financed by multilateral development institutions, including Environmental and Social Management Plan (ESMP) implementation, Resettlement Action Plan (RAP) implementation, Gender Based Violence (GBV) and Violence Against Children (VAC) supervision and monitoring and occupational health and safety aspects.
   (ii) At least five (5) years' experience in providing capacity building on techniques for development and implementation the gender issues, environmental and social safeguards documents on WB and other international financier standards.
   (iii) Experience in consultancy services related to development and monitoring of environmental and social management systems and instruments, occupational health and safety management system, grievance redress mechanism (GRM) on environment, social and gender issues supported with at least two (2) similar assignments preferred in large linear infrastructure power projects financed by multilateral development institutions.
   (iv) Must have carried out at least four (4) assignments of linear infrastructure power projects.
   (v) Preferred experience in at least two (2) linear infrastructure power projects financed by multilateral development institutions. The preferred linear infrastructure power projects financed by multilateral development institutions must be of voltage level of 220kV and above.

   Note: The consultant must prepare a Table Summary with the following information for completed linear infrastructure power projects within the last ten (10) years: (i) Project Name; (ii) Contract Number; (iii) Contract Value; (iv) Contract Signing Date; (v) Original Completion Date; (vi) Actual Completion Date and reasons if the completion date was delayed; (vii) Voltage Level (220kV and above). Please, submit experience in the linear infrastructure power projects with 220kV voltage level and above, only; (viii) Route Length; (ix) Country(ies) where the project is located; (x) Client's Name; (xi) Client's Address; (xii) Project Financier; and (xiii) Brief Description of the Scope Performed. If in the submitted experience the Firm participated as partnership/association/consortium in the Form of JV or Lead Firm or Sub-consultant, please state the role performed (Single Entity or JV or Sub-Consultant) and the details of scope executed. The higher the number of completed linear infrastructure power projects with voltage level of 220kV and above including their complexity, the higher the chance to enhance the shortlisting of the firm for submission of proposals.

(c) Demonstration of technical and managerial capability of the firm (provide only the entire Structure of the Organization/Firm, Organization Structure specific for this assignment, general qualifications, relevant number of key-staff, and list of completed projects indicating the name of the project/assignment, country, name of the Client, summary of major implemented activities, the role of the consultant i.e. single entity, member of JV or sub-consultant, contract cost and the duration of the assignment etc. Please, do not provide the Curriculum Vitae (CV) of key staff at this shortlisting stage, as the CV of Key Experts will not be evaluated at shortlisting stage, therefore, should not be submitted.

4. The attention of interested Consultants is drawn to paragraph 3.14 of the World Bank's Procurement Regulations November 2020 (Fourth Edition), setting forth the World Bank's policy on conflict of interest.

5. Consultants may associate with other firms to enhance their qualifications, but should indicate clearly whether the association is in the form of a joint venture and/or a sub-consultancy. In the case of a joint venture, all the partners in the joint venture shall be jointly and severally liable for the entire contract, if selected. Therefore, each member of JV must independently meet the requirements of the shortlisting criteria. Hence, each member of the JV shall be evaluated independently. In case one or both JV partners not meeting the shortlisting criteria stipulated under Paragraph 4 herein, then both JV partners shall forthwith be disqualified at this shortlisting stage. The Technical and Managerial Capability of the Sub-Consultant shall not be evaluated to enhance the qualification of the Applicant.

6. A Consultant will be selected in accordance with the Quality and Cost Based Selection (QCBS) method set out in the World Bank's Procurement Regulations.

7. Further information can be obtained at the address below during office hours 0800 Hours up to 1700 Hours East African Time on Monday to Friday inclusive except on public holidays:

   **Secretary TANESCO Tender Board**
   **TANESCO Office,**
   **Third Floor, Room No. A 305,**
   **Umeme Park Building,**
   **Morogoro Road, Ubungo Area**
   **P.O. Box 9024,**
   **Dar es Salaam.**
   **TANZANIA.**
   **Email: sec.tenderboard@tanesco.co.tz ;**
   **Copy: pmuprojects@taneco.co.tz**

8. For clarification purposes and, the Client's address is:

   **Secretary TANESCO Tender Board,**
   **P. O. Box 9024,**
   **Dar es Salaam - Tanzania**
   **Attn.: Ms. Rehema O. Shabani,**

   **Address:**
   **Morogoro Road, Ubungo Area, Umeme Park Building,**
   **3rd Floor, Room No. A305.**
   **City: Dar Es Salaam**
   **Country: TANZANIA**
   **Telephone: +255 222 210 231/232**
   **Email: sec.tenderboard@tanesco.co.tz**
   **Must copy the following:**
   **PMU Projects: pmuprojects@tanesco.co.tz**
   **Mr. Elias J. Makunga, elias.makunga@tanesco.co.tz**
   **Mr. Timothy Mgaya, timoth.mgaya@tanesco.co.tz**
   **Mr. David D. Mrema, david.mrema@tanesco.co.tz**
   **Mr. David Kapongo, david.kapongo@tanesco.co.tz**
   **Mr. Raymond Mbaga, raymond.mbaga@tanesco.co.tz**
   **Mr. Abdallah Awadh, abdallah.awadh@tanesco.co.tz**

9. The clarifications response and/ or addendums shall be posted on TANESCO Website: **https://tanesco.co.tz/index.php/procurement/current-tenders?own=0 for interested firms to comply.**

10. Expressions of interest must be submitted in a clearly marked envelopes and delivered to the following address (in person or by e-mail through address: taza.consulting@tanesco.co.tz) on or before Friday, 05th May, 2023 at 10:30 Hours East African Time: In addition to the original hard copy, the number of copies to be submitted with the EoI is: Two (2) hard copies and three (3) soft copies in separate USB Flash drives in read only format. Any discrepancies between the original and the copy/ or copies, the original document shall prevail. In the EoI, please, clearly state the Name of the Consulting Firm, the Physical Address, Postal Address, Valid E-mail Address, Website and Telephone Numbers. In case of association/ partnership/ consortium please, state clearly if is in the form of a Joint Venture (JV) partnership/association/consortium or is a Lead Firm with other partner/ associate/ consortium member(s) as Sub-consultant(s). For any partnership/ association/ consortium each member must provide full details of its addresses as directed hereinabove. In case of electronic submission, the original document must find TANESCO office not more than seven (7) days from the EoI Application Submission Deadline. Late submissions may be rejected.

**Secretary TANESCO Tender Board**
**TANESCO Office,**
**Ground Floor, Room No. G 04,**
**Umeme Park Building,**
**Morogoro Road, Ubungo Area**
**P.O. Box 9024,**
**Dar es Salaam.**
**Tanzania.**
**Email: (taza.consulting@tanesco.co.tz)**

**MANAGING DIRECTOR**
**TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LTD**



## Wachafuzi KINAPA kukumbana na faini

**Na Mary Mosha** MOSHI

UONGOZI wa Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro (KINAPA), umesema umeweka mpango mkakati ili kuhakikisha Mlima Kilimanjaro unakuwa msafi wakati wote na kwamba utazifungia kampuni zote ambazo watu wake watahusika kuchafua mazingira kwenye mlima huo.

Kadhalika, uongozi huo umesema kabla ya kuzifungia kampuni hizo zilizoko zaidi ya 200, utaanza kwa kuwapa adhabu wapagazi na waongoza watalii watakaobainika kufanya kosa hilo wakiwa mlimani humo.

Kwa mujibu wa Sheria ya Utalii ya mwaka 2018 iliyofanyiwa marejesho 2022, adhabu itatolewa kwa makosa yote yanayofanyika ndani ya hifadhi ikiwamo uchafuzi wa mazingira kwa kuwatoza fidia kuanzia Sh.50,000 hadi Sh. milioni moja. Hayo yalisemwa juzi na Ofisa Uhifadhi wa KINAPA, Vitus Mgaya, wakati wa kikao cha wadau wa utalii kilichofanyika Manispaa ya Moshi, mjini hapa.

"Kwa sasa kutakuwa na utaratibu wa kuhakikisha kabla ya kuondoka kituoni kwanza, usafi unafanyika kwa kuwa mnapofika kituo kingine mnakikuta ni kisafi, hivyo mkiondoka mnatakiwa kukiacha kikiwa kisafi na jambo hili tutalisimamia," alisema Mgaya.

Alisema wamelileta kwa wadau ili kupokea maoni ya namna bora ya kukabiliana na tatizo hilo ikiwa ni pamoja na kueleza mikakati ya KINAPA.

Pia alisema wamefikia hatua hiyo baada ya kuona mlima unachafuliwa bila sababu za msingi licha ya kutoa maelekezo na kuweka matangazo mbalimbali lakini baadhi yao wamekuwa wakikaidi.

"Ni aibu kuona watalii wanakuja kwa ajili ya kuangalia vivutio vilivyoko wanakumbana na uchafu ambao unasababishwa na watu wachache," alisema Mgaya.

Angela Nyaki, Mhifadhi Mkuu wa KINAPA, alisema wamelazimika kufikia uamuzi huo ili kuwakumbusha wamiliki wa kampuni za utalii wajibu wao wa kusimamia usafi katika hifadhi hiyo.

"Tunaona kutoa adhabu kwa wapagazi na waongoza watalii haitawaumiza nyie,tumeamua kuanza kufanya utafiti wa kubaini kampuni ambazo watu wake, wanachafua mazingira ya mlima huu kwa ajili ya kutoa adhabu itakayowakumbusha kuweka kipaumbele kwenye suala la usafi na sio kuangalia biashara zao pekee," alisema Nyaki.

Mmoja wa wadau walioshiriki katika kikao hicho, Emanuel Mota, alisema kutolewa kwa adhabu hiyo, kutaongeza umakini ila bado watu wanatakiwa kupewa elimu zaidi.

"Jamii yetu baadhi ya watu asilimia 70 ni wachafu na wamelelewa katika mazingira ya uchafu hivyo vizazi vinavyokuja huona uchafu kuwa ni sehemu ya kawaida,tuombe Wizara ya Maliasili na Utalii kuendelea kutoa elimu watu kuchukia uchafu kwa kuwa una madhara ili kujenga kizazi bora cha kupenda mazingira," alisema Mota.

# Mikopo ya mil. 315/- yatolewa makundi maalum kukuza uchumi

**Na Allan Isack,** ARUMERU

VIKUNDI vya wanawake, vijana na wenye ulemavu katika Halmashauri ya Meru mkoani Arusha, vimepatiwa mkopo wa Sh. milioni 315 unaotokana na makusanyo ya ndani ya halmashauri hiyo.

Katika vikundi hivyo vilivyopatiwa mkopo huo, 40 vilikuwa vya wanawake, 23 vya vijana na saba vya watu wenye ulemavu. Mikopo hiyo imetolewa ikiwa ni utekelezaji wa agizo la serikali kila halmashauri kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kuviwezesha vikundi hivyo kiuchumi.

Akizungumza jana wakati wa hafla ya utoaji wa mafunzo na kukabidhi mfano wa hundi kwa vikundi hivyo, Flora Msilu, Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, katika halmashauri hiyo, alisema wanaendelea kutekeleza kwa vitendo agizo la serikali la kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia mapato ya ndani.

Msilu alito wito kwa wanufaika wa mkopo huo,kurejesha fedha hizo ili kutoa fursa kwa watu wengine kupata mkopo kwa kuwa ni haki yao.

Kadhalika aliwataka wanufaika hao,kutumia mkopo kwa malengo waliyokusudia ikiwamo kukuza kipato cha familia, biashara wanazofanya pamoja na kujikwamua kiuchumi.

"Ndugu zangu mikopo hii tunayoichukuwa tukafanyie kazi husika tuliyokusudia kwa kuwa lengo la serikali kutoa mkopo ni kuwainua wananchi wake kiuchumi sambamba na kupambana na umaskini," alisema.

Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM) Wilaya ya Meru, Ombeni Elisante, aliwataka vijana kutumia mkopo huo,kwa tija kujikwamua kiuchumi na kushiriki katika ujenzi wa taifa.

Alisema chama hicho, kitaendelea kuisimamia serikali kwa umakini ili kuhakikisha inawaletea wananchi maendeleo kwa maslahi ya mtu mmoja mmoja na nchi kwa ujumla.

"Chama Cha Mapinduzi kitahakikisha wananchi wanapata maendeleo na utoaji wa mkopo huu kwa kuwa Ilani ya CCM Sura ya pili ibara ya 23 imelenga kuwawezesha wanawake,vijana na watu wenye ulemavu ili wajikwamue kiuchumi," alisema.



Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara, Regina Ndege (kulia), akijadiliana kuhusu masuala mbalimbali ya kimaendeleo na Diwani wa Kata ya Mirerani, wilayani Simanjiro, Salome Mnyawi, walipokutana katika kikao cha Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT), Mirerani juzi. **PICHA: GIFT THADEY.**

# Uwekezaji bandari waongeza mapato

**Na Oscar Assenga,** TANGA

NAIBU Waziri wa Uchukuzi, Atupele Mwakibete, amesema uwekezaji uliofanyika katika Bandari ya Tanga, umechangia kuongezeka kwa mapato kufikia Sh. bilioni tano kwa kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu.


Mwakibete aliyasema hayo juzi wakati wa ziara yake ya siku moja alipotembelea bandari hiyo. Alisema mapato hayo yametokana na kukamilika kwa gati, hatua ambayo imesaidia kuongezeka kwa shehena ya meli za mizigo.

Pia alisema mafanikio hayo yalitokana na uwekezaji wa takribani Sh. bilioni 429 uliofanywa na serikali kwenye bandari hiyo, hivyo kusaidia kuongezeka kwa shehena ya mizigo na kusababisha kuongezeka kwa mapato.

"Kazi nzuri ya uwekezaji ambao umefanywa na Serikali hatua hii imeleta manufaa makubwa katika bandari, nitoe wito kwa wafanyabiashara kuitumia bandari vizuri kutokana na upekee wake,""alisema.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri huyo alitoa mwezi mmoja kwa Shirika la Reli Tanzania (TRC), kuhakikisha linajenga miundombinu ya reli katika bandari hiyo ili kurahisisha huduma za usafirishaji wa mizigo inayoshushwa kuelekea maeneo mbalimbali ya nchi.

Kaimu Meneja wa Bandari ya Tanga, Peter Milanzi, alisema kwa kipindi cha miezi mitatu, wamepokea meli kubwa tano ambazo zimebeba zaidi ya shehena ya mizigo tani 130,000. Milanzi pia alisema uingiaji wa meli kubwa umesaidia kupatikana kwa ajira za muda mfupi 100 ambazo zimewawezesha wananchi kupata kipato.



# Zimamoto yakemea vibali ujenzi holela

**Na Vitus Audax,** MWANZA

JESHI la Zimamoto na Uokoaji mkoani Mwanza limekemea tabia za baadhi ya watumishi wa idara za ardhi na mipango miji wanaovunja sheria kwa kutoa vibali vya ujenzi wa makazi bila ramani kupitishwa katika jeshi hilo.

Jeshi hilo limesema inasababisha kuwapo makazi holela na wakati mwingine kusababisha kukosekana kwa miundombinu rafiki wakati wa uokoaji wa majanga.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Mrakibu Kamila Labani alisema hayo wakati wa hafla ya kuwavalisha vyeo maofisa na askari 21 wa jeshi hilo katika mkoa wa Mwanza.

Mrakibu Labani aliwataka maofisa wanaotoa vibali vya ujenzi wa nyumba kuhakikisha wamepata idhini kutoka katika jeshi hilo kama sheria inavyotaka ili kuwapa ushauri wa namna ya kuweka miundombinu ya uokoaji kabla hawajajenga makazi yao.

Pia alisema Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji namba 14 ya mwaka 2017 ikisomwa pamoja na marekebisho yake namba 8 ya mwaka 2021 kifungu cha 22(2) kimetoa maelekezo ya ramani ya ujenzi kupita katika jeshi hilo kabla ya kupewa kibali cha ujenzi na mamlaka husika.

Katika hatua nyingine, Kamanda Labani aliwataka maofisa na askari waliovalishwa vyeo kufanya kazi kwa kufuata sheria na kuzingatia viapo vyao vya utii kwa taifa ili wananchi wapate huduma wanayoitarajia kutoka katika jeshi hilo.

Baadhi ya maofisa na askari wa jeshi la hilo waliovalishwa vyeo, waliwataka wananchi kuacha tabia ya kuwaogopa pindi yanapotokea majanga hali inayosababisha majanga kuleta athari kubwa pindi yanapotokea.

"Kuna muda tunashindwa kufika katika maeneo husika kwa wakati kutokana na wahusika kutotoa taarifa kwa wakati hali inayosababisha athari kuwa kubwa zaidi kuliko pale ambapo tungepewa taarifa mapema," alisema Sajenti Sarah Yohana.



Mbunge wa Musoma Vijijini, mkoani Mara, Prof. Sospeter Muhongo (wa pili kushoto), akikabidhi msaada wa mahindi na maharage kwa Mwenyekiti wa kijiji cha Kusenyi, Abel Wambwe juzi, kwa akili ya waathirika wa mafuriko ya mvua yaliyotokea mwanzoni mwa wiki hii. Kulia ni Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kwikuyu, Raphael Ng'ombe na Mwenyekiti wa Kitongaji cha Nyabweke, Bryson Malelemba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waanza kunufaika ujenzi kituo cha afya

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

ZAIDI ya wakazi milioni moja katika mji mdogo wa Kagongwa, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wameondokana na adha ya kutembea umbali wa kilometa 30 kwenda Hospitali ya Manispaa hiyo kutafuta huduma za matibabu, baada ya serikali kuwajengea kituo cha afya kwa gharama ya Sh. milioni 500.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa kituo hicho mbele ya Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Shinyanga, Mganga Mkuu wa Manispaa ya Kahama, Dk. Josephat Shani, alisema ujenzi wa kituo kwa awamu ya kwanza umekamilika na huduma zimeanza kutolewa kwa wagonjwa wa nje (OPD).

Alisema halmashauri ilitenga Sh. bilioni 1.8 kutoka mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya Kagongwa ili kuwaondolea wananchi adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta matibabu. Alisema awamu ya kwanza ilitoa Sh. milioni 500 ambazo zimekamilisha ujenzi wa majengo ya awali na kuanza kutoa huduma.

"Ujenzi huu unafanyika kwa awamu tatu. Awamu ya kwanza ni ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD), chumba cha upasuaji, chumba cha kufulia na ununuzi wa vifaa tiba na awamu ya pili tumejenga maabara na jengo la mionzi (X-Rays) ambayo yako katika hatua za ukamilishaji," alisema Shani.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Anderson Msumba, alisema kuanzia Aprili 3, mwaka huu, huduma zingine zitatolewa huku akiahidi kuendelea kutenga fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa majengo yaliyobaki ukiwamo uzio.

Alisema wameshanunua vifaa tiba vyote vinavyohitajika na kupeleka taka watoa huduma tisa ili kuwahudumia wananchi. Alisema kituo hicho kitasaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya ambayo inahudumia zaidi ya wagonjwa 1,000 kwa siku kutoka wilaya za jirani za Msalala, Ushetu, Shinyanga, Kaliua na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Kigoma.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, aliagiza kujengwa kwa uzio wa kituo hicho ili kuzuia uvamizi wa maeneo ya umma sambamba na kumtaka Meneja wa Wakala wa Ujenzi wa Barabara za Mjini na Vijiji (TARURA) Mhandisi Job Mutagwaba, kujenga barabara inayokwenda katika eneo hilo.

"Mji huu wa Kagongwa unakua kwa kasi kulinganisha na maeneo mengine. Wekeni uzio kwenye eneo hili ili kuzuia uvamizi. Wako wananchi wanapenda kuvamia maeneo ya umma kwa maslahi yao binafsi, hivyo uzio utasaidia kuongeza usalama wa wagonjwa wanaopatiwa huduma katika kituo hiki," alisema Mndeme.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa aliwataka wananchi kuchangamkia fursa zitokanazo na mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta gafi ambalo linapita katika eneo hilo ili kujiongezea kipato ndani ya familia zao na kuachana na kurandaranda mitaani.

# Wilaya ya Nyamagana yapanda miti 400,000

**Na Ibrahimu Mmamba,** SAUT

WILAYA ya Nyamagana imefanikiwa kupanda zaidi ya miti 400,000 katika kipindi cha mwaka 2022/23 ikiwa ni sehemu ya kutekeleza agizo la serikali la kupanda miti milioni 1.5 kwa kila halmashauri kwa mwaka ili kudhibiti hewa ya ukaa.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, alisema hayo juzi wakati akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu juu ya hali ya uhifadhi wa mazingira katika wilaya hiyo.

Makilagi alisema zimekuwa zikifanyika shughuli mbalimbali katika wilaya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa mazingira ili kufikia azma ya taifa ya kila wilaya kuhakikisha inapanda miti ya kutosha kwa ajili ya uhifadhi na kudhibiti hewa ya ukaa.

Pia alisema siku ya uzinduzi wa upandaji miti walipanda miti 3,000 katika Wilaya ya Nyamagana na Makamu wa Rais, Dk. Philiph Mpango, wakati akiweka jiwe la msingi katika ujenzi wa mradi wa chanzo cha maji cha Butimba, alisisitiza upandaji miti na bado wanaendelea kuitekeleza.

"Kwa sasa tumedhamiria kuwa kila tukio linalofanywa na taasisi yoyote ile ya kiserikali au binafsi suala la upandaji miti linapewa kipaumbele na mpaka sasa ni miti zaidi ya 400,000 tutakuwa tumepanda ikifika wiki kesho," alisema.

Licha ya kuweka kipaumbele katika shughuli za upandaji miti wilayani humo, tayari wameanza kutekeleza upandaji wa maua katika maeneo mbalimbali ya jiji la Mwanza ikiwa ni pamoja na kwenye barabara kuu na barabara za mitaa lengo likiwa ni kuongeza mvuto jijini humo.

Hivi karibuni, akieleza hali ya uhifadhi, Meneja Uhifadhi Wilaya, Emmanuel Mgimwa, alisema wilaya hiyo iko katika hali nzuri ya uhifadhi sambamba na uoteshaji wa zaidi ya miche ya miti 90,000 kwa ajili ya kuigawa kwa taasisi mbalimbali ili kuendelea na zoezi la upandaji miti ili kufikia lengo la taifa.

ama
ALHAMISI APRILI 6, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Salamu za Dk. Mpango anapodai miti milioni 1.5 kwa kila halmashauri**



Ukurasa 13

Simulizi ya urafiki wa faida msaada kusafisha mazingira



Ukurasa 14

**Aliyekutwa na wakati mgumu, asimulia nafasi ya bima za afya katika kunusuru**

# Ujue undani wa ugonjwa degedege unavyoshabihiana na 'mbia' kifafa

**Na Pilly Kigome**



Mgonjwa anayesadikiwa kuwa na kifafa, akihudumiwa. **PICHA: MTANDAO**

KUNA maradhi degedege na kifafa, huwa yanawaingiza watoto na watu wazima katika hatari, yakionekana kwa sura tofauti, kulingana na hali ya mgonjwa.

### MAANA YAKE

Kuna kundi la wanajamii wanaunganisha na ushirikina. Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Watoto Hospitali ya Rufani Mkoa Temeke, Salha Ally, anataja degedege ni dalili ya mvurugano katika ufanyaji kazi wa seli za ubongo (neurons) zinazowasiliana kwa njia kama mtiririko wa umeme.

Anasema, iwapo inatokea tofauti yoyote katika ufanyaji kazi wa seli hizo za ubongo, zinakosa mtiririko huo wa asili na kusababisha degedege.

Dk. Salha anafafanua sababu zinazochangia; ikianza na kuwapo jeraha katika ubongo, linalokuwa sababu, hasa mtoto anapozaliwa.

Pia, anasema degedege inahusishwa na mabadiliko ya muda mfupi katika ubongo kama vile joto kali, matumizi ya dawa za kulevya, viwango vya juu vya sukari na sodiamu katika damu, hata kuwapo uvimbe katika ubongo.

Suala la saratani ya ubongo, matatizo ya ini na figo (matatizo ya kimetaboliki) kama vile ugonjwa wa kukojoa kiwango kikubwa zaidi, hasa aina fulani ya tindikali ya amino, kwa watoto umri chini ya mwaka mmoja.

### AINA ZAKE ZILIVYO

• Degedege la Homa; Dk. Salha anataja inawatokea kila mara watoto, akiitaja inatibika na kupona kirahisi, kuliko nyinginezo. Pia, inatajwa inaweza kuashiria hatari ya maambukizi ya bakteria mwilini (sepsis) au katika ubongo wa mtoto.

Anafafanua, degedege hiyo inasababishwa na magonjwa kama vile malaria, mashambulizi ya vimelea katika njia ya hewa, maambukizi kupitia chakula, vilevile maambukizi kwenye mkojo (UTI).

Dk. Salha anasema inawapata wenye umri kati ya miezi 6 mpaka miaka mitano, huku walio na umri miezi 14 mpaka 18, ndio wanaoongoza kuathirika.

Anasema tafiti zinaendelea kuchambua uhusiano kati ya homa kali na degedege, ingawa baadhi ya wanasayansi wanahusisha na sababu za kijenetiki.

Kunatajwa degedege lingine linalohusu kupanda ghafla joto mwilini kufikia sentigredi 39 au zaidi, ikidumu chini ya dakika 15, mtoto anatawaliwa na kizunguzungu. Hiyo hutokea wastani mara moja kwa saa 24 na haisababishi jeraha la kudumu katika ubongo.

• Degedege la homa lisilo rahisi; holo linadumu kwa zaidi ya dakika 15, ikihusisha sehemu za mwili wa mtoto na inatokea zaidi ya mara moja katika saa 24, ikiwa na uwezekano mkubwa kusababisha kifafa, siku za baadaye.

• Degedege lisilo na homa; hiyo haiambatani na homa za kila mara, ila inaashiria kuwapo tatizo katika ubongo, ikisababishwa na mtiririko mkali wa mawasiliano kati ya seli za ubongo kuwa na kasi kubwa. Huwa na tabia ya kujirudia.

Dk. Salha anashauri, mgonjwa kupimwa kiwango cha madini mwilini hasa sodiamu, sukari, au sumu. Ikitokea mara mbili au zaidi kwa saa 24, ni ishara ya ujio wa kifafa.

• Degedege la upande mmoja mwilini; hujitokeza kwa kuhusisha sehemu ya ubongo na ishara ya sehemu tu ya mwili inaonyesha dalili zake.

Aina hiyo hutokea kwa namna mbili; mtoto anaweza kupoteza fahamu asijue kinachomtokea, pasipo kupoteza fahamu.

Vilevile kuna wakati inakuwa vigumu kutambua aina hiyo ya degedege, kwa sababu huchukua muda mfupi, wastani sekunde 10 hadi 20 na kuna wakati mtoto anaweza kuongea, wakati degedege inaendelea.

Hapo huhusisha kucheza misuli usoni, shingo au sehemu za mikono hata mzazi asitambue. Ili kutofautisha na michezo, degedege inapoanza, mtoto hawezi kuizuia mpaka imalizike, hata kama mzazi utamwambia aache.

• Degedege mwili mzima; Sehemu kubwa ya ubongo huathirika na matokeo mwili wote, kuonyesha dalili anaumwa akipoteza fahamu.

Dk. Salha anaieleza kwa namna mbili; Degedege potevu, ambayo ni nadra kwa mtoto chini ya miaka mitano, zaidi ikiwahusisha wasichana na haidumu zaidi ya dakika moja.

Mgonjwa huwa hafahamu, bali anaduwaa asifanye chochote kwa sekunde kadhaa, kabla ya kurudiwa na fahamu akaendelea na shughuli zake za awali na humtokea mtoto mara nyingi kwa siku, ila nguvu ya misuli haipotei.

• Degedege ya kifafa; ni zaidi kwa watoto na inakuwa na kiashiria cha muda mfupi kabla ya kuanza. Mtaalamu anasema, kuna viashiria vinatofautiana kati ya mtoto mmoja na mwiginine, ikijenga hisia kitu kinatembea mwilini, kichefuchefu, harufu, kichwa na tumbo kuuma, kuhisi woga na mabadiliko ya ladha mdomoni.

Watoto wenye degedege,

INAENDELEA UK.14

MAZINGIRA

# Salamu za Dk. Mpango anapodai miti milioni 1.5 kwa kila halmashauri

• TFS na wadau katika 'Kijanisha Dodoma, Mkuranga, Kisarawe'

**Na Frank Monyo**

NI mara nyingi Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, amekuwa akisisitiza suala la kupanda miti kiataifa, hata akaziagiza halmashauri zote nchini kusimamia kwa karibu na kuhakikisha mazingira ya maeneo yao yanakuwa ya kijani, safi, kuvutia na endelevu.

Kauli hiyo aliyoitoa hivi karibuni, kwenye uzinduzi wa kampeni ya kupanda miti kitaifa inayoratibiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), ikihisaniwa na benki ya NMB, uzinduzi uliofanyika katika eneo la Mtumba jijini Dodoma.

Vilevile, Makamu wa Rais akatoa agizo kwa jamii hususani vijana, kupata elimu zaidi kuhusu utunzaji miti, ili kuhakikisha wanachangia katika uhifadhi wa mazingira kwa weledi, hata wakakomesha uvamizi na uharibifu wa mapori tengefu nchini, ili kuboresha hali ya mazingira nchini.

"Hatuwezi kuwa hapa tunalia na vita hii, lakini uvamizi bado unaendelea, serikali ilifanya uamuzi wa makusudi kutengeneza Jeshi Usu, kama nguvu ndogo tuambieni tuwaongezee msaada kutoka kwenye vyombo vingine," anasema Dk. Mpango.

Pia katika hilo, kimuundo wa serikali, kiongozi huyo, ofisi yake ndiyo yenye dhamana ya kusimamia ustawi wa mazingira kitaifa.

Dk, Mpango anasisitiza nafasi ya kila mmoja kuwajibika kwa nafasi yake katika upandaji miti, dhamira iliyowekwa ni kupanda miti milioni 1.5 katika kila halmashauri kwa kipindi cha mwaka mmoja itafikiwa.

Hatua hiyo, inaungwa mkono na Vodacom Tanzania Foundation kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira na Wanyamapori (WWF) kwa kutekeleza miradi ya Kijanisha mkoani Dodoma na Wilaya za Mkuranga na Kisarawe, ikiwa ni sehemu ya mipango ya kampuni hiyo kupitia shughuli za uwajibikaji kwa jamii za Kitanzania.

Mradi wa 'Kijanisha Dodoma ulizinduliwa mwaka 2019, lengo ni kuunga mkono mkakati wa serikali wa upandaji miti takribani 100,000 jijini Dodoma na kuhamasisha usimamizi endelevu wa taka mkoani humo.

Mradi wa 'Kijani Zaidi' ulianza kutekelezwa mwaka 2020, ikiwa ni jitihada za kurudisha ustawi wa misitu ya Pwani ya Vikindu na Pugu-Kazimzumbwi. kupitia uhifadhi na mpango endelevu wa utalii.



Shughuli rafiki za mazingira zikendelea wilayani Mkuranga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Ni hali anayoitaja iliendana na kunadaliwa vitalu viwili vya miti katika wilaya za Mkuranga na Kisarawe, vyenye uwezo wa kuzalisha miche mpaka 30,000.**

### WADAU NA MAFUNZO

"Miradi hii imeonyesha mafanikio makubwa kwa kufanikisha malengo yake, kama ilivyoonyeshwa kwenye ripoti ya tathmini ya mwaka 2021/2022, 'Kijanisha Dodoma' imefanikiwa kwa asilimia 85 kwa jumla ya miti 71,782 ilipandwa, kati ya 100,000 iliyotarajiwa," anasema Mkurugenzi wa Uhusiano wa Nje wa Vodacom Tanzania, Zuweina Farah

Anafafanua ni mpango unaotoa fursa za vibarua 412, wakiwamo vijana wa kiume 245 na wanawake 167. Pia, unatajwa kusaidia mapipa ya taka 10 yenye uwezo wa kuhifadhi lita 1,100 kila moja kusaidia shughuli za usimamizi wa taka ngumu na kufanikisha kujenga uzio wa waya zilizoshikiliwa na nguzo za zege za kilometa 1,129 kuzunguka Msitu wa Medeli Mjini Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Anasema, mradi pia umetoa mafunzo kwa wajasiriamali na wanawake na vijana, kuhusu ujuzi wa shughuli za kiuchumi endelevu kwa mazingira zikiwamo ubunifu na uzalishaji wa mabegi ya plastiki rafiki kwa mazingira.

Mengine yanatajwa ni; maarifa ya usimamizi wa biashara, huduma kwa wateja, na mikakati ya masoko, inayojumuisha vijana na wanawake 40,000 kutoka jamii husika, zikiwamo taasisi za elimu za mkoani Dodoma, zilihusishwa moja kwa moja wanufaika mbalimbali wakitajwa idiom yao ni zaidi 350,000.

"'Kijani Zaidi' imechangia jitihada za kurudisha ustawi wa misitu ya Vikindu na Pugu-Kazimzumbwi kupitia uhifadhi na mpango endelevu wa utalii. Vikundi vya vijana na wanawake vilipatiwa mafunzo ya kuzalisha mkaa mbadala kutoka msituni na mabaki ya shambani ikiwa ni jitihada za kukuza matumizi ya nishati safi.

"Mradi uliwapatia mafunzo ya kimkakati na kujipatia teknolojia inayofaa ya uzalishaji, ambayo iliwawezesha kutengeneza bidhaa mbalimbali, zikiwamo majiko, mikate, keki, na skonsi. Matokeo yake sasa wanawake wanaweza kujiingizia kipato cha shilingi 40,000 mpaka 60,000 kwa wiki," anasema Zuweina Farah

Anafafanua kuwa mpango huo ulilenga kuviwezesha vikundi na kukuza shughuli endelevu za kiuchumi pamoja na kuelezea changamoto ya mabadiliko ya tabianchi.

Ni hali anayoitaja iliendana na kunadaliwa vitalu viwili vya miti katika wilaya za Mkuranga na Kisarawe, vyenye uwezo wa kuzalisha miche mpaka 30,000.

"Vodacom Tanzania imetumia rasilimali zake za kampeni za kimasoko redioni na jumbe fupi za maneno kujenga hamasa na mabadiliko ya tabia kuhusu uhifadhi wa mazingira mikoani, pia ikihamasisha shughuli jumuishi za kijamii.

"Miradi yote miwili inaonyesha maendeleo chanya na imefikia malengo iliyojiwekea, kama vile kurudisha ustawi wa misitu ya Pwani kupitia uhifadhi wa Vikindu na Pugu-Kazimzumbwi, mipango endelevu wa utalii, na kuunga mkono usimamizi wa jitihada za kuifanya Dodoma kuwa ya kijani" anasema na kuongeza:

"Ikiwa imetekelezwa kwa ushirikiano wa karibu na serikali, mafanikio ya miradi hii inaonyesha umuhimu wa kuhamasisha na kuunga mkono jitihada za kuongeza hamasa kuhusu mabadiliko ya tabianchi, athari zake, na kuzizungumzia.

"Umuhimu wa ushirikiano baina ya serikali na taasisi binafsi kukusanya rasilimali na kupanua miradi ya aina hii nchini kote, kwa kuchukua hatua muhimu kuelezea changamoto za mabadiliko ya tabianchi, tunaweza kufanikisha lengo la mpango endelevu wa dunia na kutengeneza mustakabali wa dunia yetu," anasema.

### MKUTANO WA COP27

Vodafone, ambayo ni kampuni mama ya Vodacom Tanzania, ilitangazwa kuwa mshirika Mkuu wa Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Umoja wa Mataifa (COP27) ulioandaliwa na serikali ya Misri mwaka jana, ikwa ni hatua ya mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi na athari zake, katika kufikia kufikisha lengo la maendeleo endelevu ya dunia kufika 2030.

Pendekezo la shirika hilo, ni kuzijumuisha huduma na teknolojia muhimu kwenye mifumo ya kidigitali, kama vile 'mtandao jumuishi wa shughuli kwenye intaneti,' unaweza kuzisaidia jamii kutunza nishati, kutengeneza miji Rafiki kwa mazingira, na kuongeza ufanisi wa sekta tofauti za kiuchumi kama vile usafirishaji na kilimo.

Kwa kuzingatia mafanikio hayo, sasa uinatajwa ni muhimu kukuza na kuunga mkono miradi yite inayoongeza hamasa kuhusu mabadiliko ya tabianchi, athari zake, na suluhisho.

AFYA

KUTOKA HOSPITALINI OCEAN ROAD...

# Simulizi ya urafiki wa faida msaada kusafisha mazingira

**Na Beatrice Moses**

KATIKA dhana ya urafiki, daima upo wa namna tofauti, kama vile wa mtu na mtu, familia, taasisi na hata nchi. Msingi wake mkuu ni upendo na ushirikiano katika kupata ufumbuzi wa mambo kadhaa, kufurahi na kutoa faraja kwenye huzuni.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, kampuni ya Weka Jiji Safi (WEJISA) inayojihusisha na masuala ya usafi hasa wa nje ya majengo, barabarani na miferejini, kwa kutambua umuhimu wa marafiki, iliamua kuwaalika wadau wake kushirikiana nao, katika kufanya usafi kwenye Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, jijini Dar es Salaam.

WEJISA iliwaalika wadau wake kama Klabu ya Waandishi wa Habari mkoa wa Dar es Salaam (DCPC), Dar Lions Club, Shika Fagio na wengine, kujumuika nao katika kusafisha mazingira yanayoizunguka taasisi hiyo, pia kutoa misaada mbalimbali kwa wagonjwa.

"Tenganisha Taka, Okoa Mazingira" na "Tenganisha Taka, Okoa Rasilimali" ndiyo kaulimbiu zilizoongoza shughuli hiyo, ambayo Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, alialikwa kuwa mgeni rasmi, lakini aliwakilishwa na Ofisa Tarafa wa Kariakoo, Christina Kalekezi.

Kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya, Kalekezi anatumia nafasi hiyo kuwashukuru WEJISA na wadau wengine kujumuika, kwa kuona umuhimu wa kufanya usafi katika hospitali hiyo, kwa kuwa ni hatua njema inayolenga kuhakikisha mazingira ya wagonjwa, madaktari, wafanyakazi na ndugu au jamaa wanaofika hapo yanakuwa salama.

Kalekezi anasema usafi ni ibada na kufanya usafi hapo hospitalini kunawasaidia watu waliopo katika eneo, wakafikiwa na hewa safi, hivyo kunazuia kuzuka magonjwa yanayosababishwa na uchafu.

Pia, anatumia nafasi hiyo kupongeza ukusanyaji wa taka katika mtindo wa kuzitenganisha, hatua ambayo anaielezea inasaidia kupunguza mrundikano wa taka kwenye dampo.

"Hatua hiyo inasaidia pia kupunguza mabadiliko ya tabianchi, ambayo hutokea iwapo kunakuwa na mrudikano wa taka uliokithiri,"anatamka na kuongeza.

"Nawapongeza kwa hatua hii nzuri, kama hivyo kutenganisha taka ni jambo jema, siyo taka zote ni taka, zipo nyingine zinazotumika katika matumizi mengine yenye faida pia."



Baadhi ya marafiki wadau waliojitokeza kufanya usafi wa mazingira katika Taasisi ya Kansa Ocean Road iliyopo jijini Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: BEATRICE MOSES**

> **Nawapongeza kwa hatua hii nzuri, kama hivyo kutenganisha taka ni jambo jema, siyo taka zote ni taka, zipo nyingine zinazotumika katika matumizi mengine yenye faida pia.**




### KUTOKA WEJISA

Meneja Mwendeshaji wa kampuni ya WEJISA, Ally Kunambi, anabainisha kwamba ndani ya taka kuna fursa za kiuchumi, ambayo baadhi ya wadau baada ya kuzitenganisha zinayeyushwa kuwa bidhaa nyingine na zile za vyakula zinatumika kutengeneza mbolea.

Anasema baada ya kulibaini hilo, kampuni yao ya usafi imekuwa ikijitahidi kuhakikisha uzoaji wa taka unazingatia katika kutenganisha, kwa kuziweka taka ngumu pekee, dhidi ya zile za mabaki ya vyakula nazo zinawekwa kwenye vifaa maalum vya kuhifadhi taka husika.

"Takataka ni fursa zinatumika kwenye matumizi mengine kulingana na aina ya taka zenyewe. Hivyo, tunazingatia kutenganisha takataka hizo, pia tunalenga kuzuia magonjwa kwa taka hatarishi zinawekwa kwenye vifaa tofauti," anasema Kunambi.

Ofisa Afya wa serikali, Abdallah Mrindoko aliyeshiriki kwenye usafi huo, anasema faida kubwa katika kusafisha mazingira inasaidia ama kuharibu au kuondoa mazalia ya wadudu wanaosababisha magonjwa kama vile inzi, mende na mbu.

### WADAU WA TUKIO

Katibu Mkuu wa DCPC, Fatma Jalala, anasema klabu hiyo imefurahi kushirikishwa katika usafi wa hospitali hiyo kwa kuwa ni sehemu ya kuitumikia jamii, kwa kuwa wao wanahabari wana jukumu la kuhakikisha pia habari nzuri zinazosaidia kulinda afya za wanajamii na kuiletea maendeleo zinapewa kipaumbele.

"DCPC tupo kwa ajili ya jamii, sisi ni wanahabari, tuna uwezo wa kufikisha kaulimbiu nzuri kwa jamii, hivyo tunawakaribisha wadau wengine wajitokeze kushirikiana nasi DCPC katika shughuli za kijamii, wanahabari ni kioo.

"Tunashukuru kujumuika na wenzetu WEJISA, Lions Club na wadau wengine katika zoezi la usafi, kwani waandishi ni kioo katika jamii, hivyo mbali ya kuripoti matukio, pia tunaweza kufanya kwa vitendo na kuigusa jamii kama hivi tukishirikiana na wadau" anasema Fatma.

Mwanamazingira, Castro Kayombo, kutoka MBRG the Ocean, anasema suala la kusafisha mazingira na kutenganisha taka, linapaswa kufanywa kuanzia kwenye ngazi ya familia.

" Kwa takwimu zilizopo, tani zinazozalishwa Dar es Salaam kwa siku ni 2500 na katika hizo, ni asilimia 50 pekee ndiyo zinakusanywa kwa usahihi, hivyo kuna haja ya kuendelea kuhamasishana kutunza mazingira na kutenganisha taka katika hali sahihi, itakayowezesha fursa za kiuchumi kupatikana," anasema,

Mkurugenzi wa Wejisa, Nuru Hassan, anatumia nafasi hiyo kuwashukuru wadau wao kuitikia wito kuifanya kazi hiyo, akibainisha malipo yao yatatolewa katika nguzo za imani.

Ni shughuli iliyoendana na kutolewa vyeti vya kutambua ushirikiano wa marafiki hao, kisha kukabidhi misaada kwa wagonjwa, ikiwamo dawa, sabuni, pampasi, nguo na maji.

### WENYEJI HOSPITALINI

Dk. Asafu Munema, Meneja Huduma za Maabara, akimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, anasema ni jambo la faraja kuona wanajamii wanahamasishana kukumbuka kuwasaidia kwa hali na mali wagonjwa wanaowahudumia, ambao wana mahitaji mbalimbali.

Anasema wagonjwa waliolazwa kwenye taasisi hiyo wapo ambao kutokana na aina ya matibabu, wanakaa hospitalini muda mrefu, hivyo ni wazi wakikumbukwa na wanajamii wanafarijika kwa namna yake.

"Misaada hii inawatia moyo na kuona kuwa jamii inawathamini, ni vyema kukumbukana kwa kuwa hakuna mwenye uhakika na afya yake, siku yoyote unaweza kujikuta nawe umekuwa mgonjwa hivyo ni vyema kukumbukana," anasema Dk.Munema.

AFYA

# Aliyekutwa na wakati mgumu, asimulia nafasi ya bima za afya katika kunusuru

**Na Elizabeth Zaya**

MARA zote mtu anapougua na kukutana na misukosko yake, ikiwamo gharama, mara moja anakumbuka nafasi ya kuwa na huduma ya bima ya afya.

Undani wa pilika na thamani ya bima ya afya, inaangukia katika simulizi ya maisha ya Mama Petra Kajula, mama wa nyumbani na mzazi aliyejifungua hivi karibuni.

Anasema, akiwa mjamzito mwaka jana, daktari wake alimwambia angejifungua kwa njia ya upasuaji, hivyo anapaswa kujiandaa kifedha, kukabili haja hiyo.

Petra baada ya kupewa taarifa hizo, anasema zilimchanganya sana, hasa ikizingatiwa ukubwa wa gharama za kujifungua kwa njia ya upasuaji.

Mama huyo anayemtambulisha mume wake ni dereva wa bodaboda na uchumi wao uko chini, anasimulia taarifa hizo na daktari zilimpa wakati mgumu, akiwaza moja kwa moja uwezekano wa wao kumudu gharama za upasuaji ulivyo mdogo.

Akafafanua kipato chao, kilitosha kulipia gharama zao za maisha za kila siku pekee. Petra anaeleza kwamba mwezi aliotarajia kujifungua ulikuwa umekaribia na wakati anapata taarifa hizo, familia yake ilikuwa imejiandikisha katika Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (CHF), tangu mwaka 2021, lakini walikuwa bado hawajalipia.

Uamuzi waliofikia na mumewe, wakapambana na kufanikiwa kulipia, huku akikiri kwamba, kabla ya kujiandikisha walikuwa hawaoni umuhimu wa kujiandikisha kwenye bima hiyo, ile picha kamili ya thamani ya bima, ikajionyesha penye hitaji la kiafya lilipochukua nafasi.



Petra Kajula, akiwa na mwanawe, akijivunia bima ya afya. **PICHA: ELIZABETH ZAYA.**

"Kwa hiyo ni muhimu sana watu kujiandikisha na kupatiwa bima ya afya kwa sababu inasaidia kupunguza gharama tofauti na ambavyo ukikumbwa na magonjwa, unatumia fedha nyingi kama hakuna msaada wa bima," anasimulia Petra.

Anaendelea: "Nimekuwa shuhuda wa hili na nashukuru imenirahisishia katika hatua yangu ya kujifungua ambayo ilikuwa ni kwa upasuaji."

### MRATIBU CHF

Bernard Shaba, Mratibu wa Bima ya 'CHF' katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, anakoishi Petra, anasema awali hapakuwapo mwitikio wa kutosha wa wananchi kujiunga na bima ya afya, hasa kutokana na kukosekana taarifa za kutosha kuhusu umuhimu wa bima.

Anasema tayari wameanza kufanya jitihada za kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa bima ya afya kwa njia mbalimbali, ikiwamo kupitia vipindi vya redio za jamii.

"Watu wachache sana walikuwa wanajiunga bima ya afya kwa sababu hapakuwa na taarifa za kutosha, lakini baada ya vipindi vya redio, watu wengi sasa wameanza kufahamu jambo hili.

"Hata tunavyozungumza, ongezeko la watu wanaoomba kujiunga bima kwa sasa ni kubwa, lakini pamoja na mwitikio huo tunaouona, tutaendelea kutoa elimu zaidi," anasema.

### NGUVU YA UWEZESHAJI

Ni mradi unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI), zikiwezesha mamlaka za serikali za mitaa, kuhakikisha kunatolewa elimu kuhusu umuhimu wa kila mwananchi kuwa na bima ya afya.

Ni mpango unaopitia uwezeshaji kielimu kupitia vipindi vya redio binafsi za kijamii, imeongeza mwamko na uelewa wa wananchi wengi hususani walio vijijini kujiandikisha na kupata bima ya afya.

Ina maudhui ya kuzisaidia mamlaka za serikali za mitaa na vyombo vya habari, kukitengwa ujumbe maalumu unaohakikisha walau vipindi 20 vinarushwa hewani, lengo ni kuwafikia zaidi ya watu milioni nne katika mikoa saba ya Tanzania Bara.

Hapo ni kwamba kumeongeza usikilizwaji redio za jamii na kusaidia halmashauri kueneza ujumbe muhimu unaohusiana na bima ya afya na huduma nyingine za umma.

Almasi Katuba, mkulima kutoka wilayani Rungwe, mkoa wa Mbeya, anasema: "Elimu kuhusu bima hii, niliisikia kwenye redio ya hapa kwetu. Kabla ya hapo nilikuwa nauza hadi mifugo yangu ikiwamo ng`ombe ili nipate fedha ya kunisaidia kwenye matibabu na wakati mwingine unafilisika, unabaki masikini kwa ajili ya kuuza vitu kugharimia matibabu hayo."

Akizungumzia suala hilo, Mkurugenzi wa Huduma za Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii (TAMISEMI), Dk. Ntuli Kapologwe, anasema asilimia 86 ya wananchi hawajajiunga na bima ya afya nchini, kutokana na kukosa elimu sahihi ya umuhimu wake.

Anasema, kwa sasa serikali iko kwenye mchakato wa kuanzisha Bima ya Afya kwa Wote ya Mwaka 2022, ikiwa katika hatua ya subira ya bunge kupitisha muswada kuwa sheria.

Mnamo Novemba mwaka jana, Bunge lilirejesha muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote mwaka 2022 kwa Kamati ya huduma za Maendeleo ya Jamii kwa mashauriano zaidi.

Kupitia Sheria inayopendekezwa, inatarajiwa kuruhusu kuwapo kwa skimu binafsi za Bima ya Afya ambazo zitatoa huduma za Bima ya Afya kwa wananchi katika sekta rasmi binafsi na isiyo rasmi. Pia, inampa nafasi waziri mwenye dhamana ya masuala ya afya, kupitia kanuni na kuweka viwango vya uchangiaji kwa kuzingatia uhitaji wa huduma, gharama halisi za matibabu na uwezo wa wananchi kuchangia.

Kadhalika, kuna wasio na uwezo watakuwa na haki ya kupata huduma za matibabu kupitia utaratibu utakaowekwa na serikali baada ya kuwatambua kupitia mfumo maalumu wa utambuzi utakaowekwa.

## Ujue undani wa ugonjwa degedege unavyoshabihiana na 'mbia' kifafa

**INATOKA UK.11**

wanakuwa na viashiria vinavyowapata na inakuwa rahisi kwao kukimbia, kuliko salama kabla ya degedege kuanza.

Madhara yalivyo, mtoto anapopoteza fahamu, wengine hutoa sauti na kugeuza macho au kuchezesha misuli ya mwili mzima ikikamaa.

Wakati degedege kwa mtoto, anaweza kuung'ata ulimi, kukojoa na wakati mwingine haja kubwa. Baada ya degedege, mhusika anadumu na hali hiyo kwa dakika kadhaa, anabaki katika usingizi, takribani nusu saa au zaidi.

• Degedege la wachanga; inatajwa kuwapata zaidi wenye umri chini ya siku 28, kwa sababu mbalimbali kama maambukizi ya vimelea vya magonjwa, matatizo ya kimaumbile na sumu mwilini.

Mara nyingi wanakuwa kama wanatafuna kitu, wakati mwingine macho kuyaelekeza upande mmoja bila ya kuyachezesha huku wakiwa wamekakamaa, pia wanaweza kuchezesha miguu kama wanaendesha baiskeli, vilevile kujionyesha kwa kubadilika rangi, au kutopumua kwa muda.

• Degedege linalodumu; aina hiyo inatajwa ni hatari zaidi na degedege humpata mtoto kwa zaidi ya dakika 30, pasipo fahamu zake.

### DALILI ZILIVYO

Dalili za degedege huonekana katika sehemu tofauti mwilini, ikihusisha sehemu mojawapo mwilini, kwenye misuli ya upande kucheza, kukakamaa au inaweza kuhusisha mwili wote.

Pia, inatajwa kuambatana na kupotea fahamu kwa mtoto. Kuna baadhi ni ngumu kutambua inapotokea na degedege hutofautiana, kutegemea na umri wa mtoto.

Mtoto anapoteza fahamu, akiwa katika hisia kama za woga na hofu isiyoelezeka, ikijenga furaha iliyopitiliza au kicheko kisicho na maelezo.

### KIJUE KIFAFA

Ni ugonjwa unaofanana na degedege. Kifafa kinasababishwa na seli katika mishipa ya fahamu kwenye ubongo zinazotoa umeme, mwingi kuliko kawaida, kwenda kwenye misuli na sehemu zingine za mwili.

Hiyo inatajwa kusababisha mtu kupata dalili kama za kuishiwa nguvu, kichwa kuuma sana, kuchanganyikiwa, mwili kukamaa na hata kupoteza fahamu.

Dk. Salha anasema ugonjwa chanzo chake kikuu hakifahamiki, ila kuna sababu kama urithi kifamilia; ajali inayodhuru mishipa ya fahamu; kuugua muda mrefu mfumo wa ubongo ukapoteza uwezo; uvimbe kwenye ubongo, kiharusi, pia magonjwa ya uzeeni.

Aina za kifafa, zinatajwa ni ya mtu anakakamaa mwili mzima na akipoteza fahamu, kutoa povu au kupata hajakubwa na ndogo bila kujitambua.

Pia, kuna ambayo mgonjwa hapotezi fahamu wala hakakamai, bali anapatwa na hali fulani ya bumbuwazi kwa dakika kadhaa, kizunguzungu na kichwa kuuma.



# Walimu watakiwa kuwa na uthubutu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WALIMU wastaafu wametakiwa kuwa na uthubutu katika kutambua fursa na kuzipangia mikakati ili kufanya miradi mbalimbali ya uzalishaji mali na kujiinua kiuchumi.

Akizungumza wakati wa mafunzo ya namna ya kutumia huduma za benki ili kujipatia mikopo kwa ajili ya ujasiriamali, Ofisa kutoka Tanzania Commercial Bank (TCB), Edward Mlowo, alisema wastaafu wanatakiwa kutambua fursa ili kuwa na uthubutu wa kufanya shughuli za uzalishaji mali zitakazowaingizia kipato.

Alisema ni vyema wakajikita kwenye shughuli za uzalishaji mali ili kujiongezea kipato na kuwawezesha kujiimarisha kiuchumi kupitia shughuli mbalimbali ambazo wanafanya.

"Hamtakiwi kukata tamaa kuzitafuta fursa. Kinachotakiwa ni kupambana na kuhakikisha mnapata matokeo chanya," alisema Mlowo.

Alisema kikwazo kikubwa ni kwamba fedha nyingi hazifiki benki na watu wengi hawatumii benki ambazo pia zina uwezo wa kuwakopesha kwa ajili ya kufanya biashara, hivyo wajiwekee utaratibu wa kutumia benki kuhifadhi fedha zao.

Pia aliwataka walimu hao wastaafu kutambua fursa na kuipangia mikakati ya uzalishaji kwenye kilimo, ufugaji au kufanya biashara za aina mbalimbali.

Katibu wa Chama cha Walimu Wastaafu Mkoa wa Dodoma, James Chagula, alisema lengo la mafunzo hayo ni kukuza uwezo wa kipato kwa walimu wastaafu ili kufanya miradi mbalimbali.

Alisema walimu wastaafu wamekuwa wakijishughulisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi, hivyo ni vyema kama wakapatiwa mafunzo jinsi ya kuona fursa zilizo katika benki na namna ya kupata mikopo itakayoongeza vipato vyao.

Mmoja wa walimu wastaafu, Avelina Chapote, alisema amekuwa akijishughulisha na ufugaji wa ng'ombe na kuku, hivyo elimu aliyoipata itasaidia kukuza biashara yake.

Alisema mafunzo aliyoyapata kutoka benki hiyo anamini anakwenda kupiga hatua katika ufugaji kuku ambao anafanya.

# Majaliwa akerwa na mmomonyoko maadili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameeleza kukerwa na kukithiri kwa vitendo vya mmomonyoko wa maadili ambavyo haviendani na mila na desturi za kitanzania huku akiagiza hatua kali zichukuliwe kukomesha hali hiyo.

Majaliwa alisema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa 13 wa Umoja wa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania (TOA).

"Vitendo vya mmomonyoko wa maadili nchini pamoja na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto vimekithiri sana nchini hivi sasa nawaomba makatibu tawala na wakurugenzi nendeni mkahakikishe mnavikomesha na kwa wale watakaobainika chukueni hatua mara moja.

"Nyie ndio ambao mnatoa vibali vya biashara lazima mjiridhishe biashara zinazofanyika katika maeneo yenu kama zinazingatia mila na desturi zetu ambazo zinaweza kuharibu vijana wetu. Pia mnapaswa kuchukua hatua mara moja kwa watakaobainika kuwa sababu ya mmomonyoko wa maadili," alisema.

Majaliwa pia alitoa maagizo kwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuhakikisha Sera ya Taifa ya Ugatuaji wa Madaraka inakamilika mara moja ili iwezeshe taasisi zote nchini kupata mwongozo wa namna ya kutekeleza dhana hiyo muhimu kwa utoaji wa huduma na maendeleo ya wananchi.

"Ofisi ya Rais - TAMISEMI iendelee kufanya kazi kwa pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango kushughulikia suala la ruzuku ya serikali za mitaa (LGDG) sambamba na utatuzi wa changamoto mbalimbali za utekelezaji wa miradi katika mamlaka za serikali za mitaa na mikoa," alisema.

Kadhalika, aliiagiza TOA kuendelea kuweka mikakati ya kuwajengea uwezo wanachama katika kuimarisha utawala bora na utawala wa sheria ikiwa ni pamoja na mifumo ya utatuzi wa migogoro sambamba na ushirikishaji wananchi katika maamuzi na mipango ya maendeleo.

Pia aliagiza TOA iwajibike kuhimiza wanachama kuhakikisha mamlaka za serikali za mitaa zinatoa taarifa za utekelezaji wa mipango na bajeti ikiwemo taarifa za mapato na matumizi ili kujenga imani ya wananchi kwa serikali yao.

"TOA itoe kipaumbele kuwawezesha wanachama katika kuandaa mikakati ya usimamizi wa miradi ya maendeleo katika mamlaka za serikali za mitaa ili kazi zinazofanywa ziwe na ubora na zilingane na fedha inayotumika.

"Kwa nafasi zenu wekeni mikakati ya ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya ndani ili kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii. Hii iwe sambamba na kubuni vyanzo vipya vya mapato, kufanya mapitio ya viwango vya ushuru na kuwa na takwimu sahihi za walipa kodi," alisisitiza.

Awali Mwenyeti wa TOA Taifa, Albert Msovela, akitoa taarifa ya umoja huo, alisema kuwa lengo lao ni kuendelea kuishari serikali katika masula ya ugatuia wa madara ili kuwashirikisha wananchi katibu uibuaji wa miradi kuanzia ngazi ya chini.

"Dhana ya ugatuia wa madaraka inatija kubwa kutokana na kuwashirikisha wanachi kuibua miradi na kutatua chanamoto zao kwa kutumia rasilimali zinazowazunguka," alisema.

Alisema pamoja na mafanikio waliyopata, bado kuna kero ambazo wanakabiliana nazo ikiwamo kukosekana kwa sera ya taifa ya ugatuaji wa madaraka, kuondolewa kwa ruzuku ya serikali za mitaa (LGDG) na uhaba wa watumishi katika mamlaka za serikali za mitaa.




Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande (kulia), akipokea taarifa ya matokeo ya ufuatiliaji na tathimini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kupitia fedha za UVIKO 19 kutoka kwa Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Prof. William Mwigoha, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Tathmini yabaini fedha UVIKO kutumika kama ilivyokusudiwa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

TATHMINI iliyotolewa na Chuo Kikuu Mzumbe inaonyesha kuwa fedha za mkopo za UVIKO- 19 zimetumika vizuri na utekelezaji wa miradi mbalimbali iliyokusudiwa imekamilika kwa wakati.

Prof. Henry Mollel kutoka Chuo Kikuu Mzumbe alisema hayo juzi wakati wa kuwasilisha taarifa ya tathmini hiyo iliyokabidhiwa kwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, jijini hapa.

Alisema chuo hicho kilikabidhiwa jukumu la kufanya tathmini ya fedha za mikopo za UVIKO-19 na kubaini kuwa zilitumika vizuri na utekelezaji wa miradi mingi ulikamilika kwa wakati. Kwa mujibu wa Prof. Mollel, serikali iliwapa kazi ya kupitia kituo cha umahiri katika ufuatiliaji na tathimini ya mifumo ya afya, ndicho kilichokasimiwa jukumu la kufanya ufuatiliaji na tathimini ya miradi iliyotekelezwa kupitia mpango huo.

Prof Mollel alisema tathmini hiyo ilihusisha uhakiki wa miradi na kufanya mahojiano na wawakilishi kutoka taasisi za utekelezaji wa miradi na ulifanyika katika halmashauri 184 nchini.

Pia alisema mradi huo ulikuwa unatekelezwa katika sekta ya afya ,maji, elimu, utalii na Ofisi ya Rais kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) huku Wizara ya Fedha na Mipango ikiwa msimamizi wa utekelezaji.

Tathmini hiyo, alisema imebaini kuwa uweao wa miradi hiyo umesaidia kupunguza upungufu wa vyumba vya madarasa na kuongeza upatikanaji wa huduma mbalimbali.

Kadhalika, alisema kuna baadhi ya miradi ilishindwa kukamilika kwa wakati kutokana na kupanda kwa gharama za vifaa vya ujenzi.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, alisema serikali ilipata mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Kimarekani bilioni 56.25 sawa na Sh. trilioni 1, 291.74 kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa ajili ya kupunguza athari za kijamii na kiuchumi kutokana na janga la UVIKO-19.

Chande alisema kati ya fedha hizo sekta ya afya ilipata Sh. bilioni 448.79 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya wagonjwa mahututi 72, ujenzi wa idara za matibabu ya dharura 101, kitengo cha wagonjwa wa nje (OPD) na wodi za wazazi, nyumba za wafanyakazi 178 na ununuzi wa vifaa na vifaa tiba na magari 103.





# Shule taabani uchakavu wa miundombinu

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

SHULE ya Msingi Melele iliyoko Kijiji cha Utengule- Usangu, Mbarali mkoani Mbeya, inakabiliwa na uhaba wa vyumba vya madarasa, nyumba za walimu na matundu ya vyoo.

Hali hiyo inasababisha mazingira magumu kwa wanafunzi kupata elimu katika shule hiyo.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Melele, Abdul Udamwa, alisema jana kuwa shule hiyo kwa sasa ina hali mbaya kutokana na uchakavu wa miundombinu, huku akisema uhaba wa madawati, vyumba vya madarasa na nyumba za walimu ikiwa ni kikwazo kikubwa kwa utoaji wa elimu shuleni hapo.

"Shule yetu ina madawati 97 lakini mahitaji ni madawati 142, upungufu ni 45. Vyumba vilivyopo ni saba wakati uhitaji ni madarasa 11, vyoo vya wanafunzi vilivyopo ni matundu matatu mahitaji ni 12. Vilevile kuna nyumba moja ya mwalimu lakini uhitaji ni nyumba tisa," alisema Udamwa.

Katika kutafuta suluhu ya vikwazo hivyo, alisema wananchi kwa kutumia nguvu zao, wamejenga nyumba moja ya mwalimu huku Mbunge wa Viti Maalum, Bahati Ndigo, akitoa mabati 40 kwa ajili ya kuiezeka.

Msaada huo ulikabidhiwa na Diwani wa Utengule- Usangu, Samora Msonsa, na kwamba mabati hayo yatatumika kuezeka nyumba moja ya walimu ambayo ujenzi unaendelea kwa nguvu ya wananchi.

Baadhi ya wananchi, akiwamo Zaud Mwalalila, alisema mabati hayo yatasaidia kukamilisha ujenzi licha ya kuwa bado wanahitaji mifuko ya saruji, madirisha, milango, choo na jiko.

Aliiomba serikali kusaidia ujenzi wa nyumba ya mwalimu mkuu ili aweze kuhamia ili kuwa jirani na mazingira ya shule.




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Dk. Venance Mwasse (wa pili kulia), akibadilishana hati na Meneja Mwandamizi wa Biashara wa Benki ya Azania, Jackson Lohay, baada ya kutiliana saini mkataba wa makubaliano ili kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata mikopo na msaada wa kitaalamu, wakati wa mkutano wa wachimbaji wadogo wa madini, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Meneja wa Benki ya Azania, Rhoda Baluhya (kushoto), Mkuu wa Idara ya Sheria Stamico, Mudrikat Kiobya (kulia) na (katikati) ni Mwenyekiti wa Bodi Stamico, Meja Jenerali, Michael Isamuhyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Hospitali rufani yapatiwa vifaa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

UONGOZI wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, umepokea msaada wa kompyuta saba kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi idara ya uhandisi ambayo ina jukumu la kuhifadhi taarifa zote za wagonjwa na mifumo yote ya mawasiliano.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Godlove Mbwanji, alisema jana kuwa kuwa vifaa hivyo vitasaidia kukabiliana na uhaba wa vitendea kazi kwenye kitengo cha uhandisi ambacho ni muhimu kwa ajili ya kuendesha shughuli za hospitali ikiwamo kutunza nyaraka zote.

Dk. Mbwanji alisema msaada huo ni mwendelezo wa ushirikiano katika kuboresha miundo mbinu na vitendea kazi katika kitengo cha uhandisi cha hospitali.

"Tunawashukuru Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) Mbeya na shirika la CHAI kwa jinsi wanavyotupa ushirikiano na leo (jana) tumepata vifaa hivi kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi. Nawaahidi vitatumika kama ilivyokusudiwa na kuleta tija katika huduma tunazozitoa," alisema Dk. Mbwanji.

Mkurugenzi wa NIMR Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (NIMR) Mbeya, Dk. Nyanda Ntinginya, alisema msaada huo umelenga kusaidia hospitali hiyo kuboresha mazingira ya kutolea huduma za matibabu kwa wananchi.

"NIMR kwa kushirikiana na Shirika lisilokuwa la kiserikali la The Clinton Health Access Initiative (CHAI) tumetoa kompyuta hizo kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi hospitali ya Rufaa ili kuendela kutoa huduma bora za afya kwa wananchi alisema Dk. Nyanda.

Fundi Vifaa Tiba kutoka Idara ya Uhandisi hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya, Esther Kikoti, alisema kompyuta hizo zitaongeza ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

# Mtoto wea kiume kutengwa chanzo ukatili

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WADAU wa kupinga ukatili wa kijinsia mkoani Mbeya, wamesema juhudi kubwa zimewekezwa kutetea na kulinda haki za mtoto wa kike huku mtoto wa kiume akisahaulika hali iliyosababisha vijana wengi wa kiume kuingia kwenye hatari kubwa ya kufanyiwa ukatili.

Walizungumza hayo jana wakati shirika lisilo la kiserikali la Sauti ya Mama Afrika (SAMAFO) likitoa msaada wa mahitaji mbalimbali kwa wajane 34 wa kata ya Nsalala wilaya ya Mbeya ikiwa ni zawadi katika kuelekea sikukuu ya Pasaka.

Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto Wilaya ya Kipolisi Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, Mary Gumbo, alisema pamoja na serikali kufanya kazi kubwa ya kukabiliana na vitendo vya ukatili, kila mmoja anapaswa kuwajibika kukabiliana na vitendo hivyo na kwamba juhudi hizo zinapaswa kuelekezwa kwa watoto wote wa kike na kiume.

"Katika kesi nyingi tunazopokea tunagundua chanzo kikubwa cha ukatili wa kijinsia ni kukosekana kwa malezi bora, hivyo wazazi na walezi wanayo nafasi kubwa ya kupunguza vitendo hivyo ikiwa watasimamia majukumu yao ipasavyo," alisema Gumbo.

Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Mbeya Vijijini, Subilaga Mwangoka, alisema watoto wa kike walionekana kuathiriwa na vitendo vya ukatili kwa kiasi kikubwa ndiyo maana uilisababisha serikali na wadau mbalimbali kuwekeza nguvu kubwa kutetea na kulinda haki za mtoto wa kike.

"Lakini sasa, alisema hali imebadilika na watoto wengi wa kiume wanafanyiwa vitendo vya ukatili, hivyo tuanze kutetea na kulinda haki za watoto wote," alisema. Asha Yongo, kutoka Kituo cha Taarifa na Maarifa kata ya Nsalala, alisema katika eneo la Mbalizi, matukio ya ukatili kwa watoto yamekithiri kutokana na wazazi na walezi wengi wa eneo hilo kujikita kwenye shughuli za kiuchumi pekee na kusahau jukumu la malezi kwa watoto wao.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo, Mkurugenzi wa SAMAFO, Tabita Bugali, alisema walitoa msaada wa mavazi, sabuni na chumvi kwa wajane 34 wa kata hiyo ikiwa ni sehemu ya kuwafariji katika msimu huu wa Pasaka huku akiahidi shirika hilo kushirikiana na serikali kupinga vitendo vyote vilivyo kinyume na maadili ya Kitanzania.

"Tumesikia kwenye vyombo vya habari baadhi ya wadau kutetea vitendo vya ushoga ,nashauri Serikali ifanye utafiti na kuwachukulia hatua wahusika.

Pia viongozi wetu wa madhehebu ya Kikristo na Kiislamu,tuwe na maombi maalumu kwa ajili ya kuombea suala hili sisi tutashirikiana na Serikali kuhakikisha maadili ya kitanzania yanalindwa na watoto wanakua salama," alisema.



## Wadau habari walia na sheria kandamizi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WADAU wa habari Zanzibar wamesema Sheria ya Adhabu Namba 6 ya mwaka 2004 ni miongoni mwa sheria zinazokandamiza uhuru wa habari, hivyo inahitaji kufanyiwa marekebisho.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti wadau hao walisema kipengele cha 44 (1) cha sheria hiyo, kinaeleza kuwa mtu yeyote bila dharura ya kisheria amechapa, amesambaza au kutoa maneno yasiyoridhisha katika mkusanyiko wowote, ni uchochezi wakati ilipaswa kuwa wazi ni maneno gani ambayo ni uchochezi.

Maulid Suleiman, Mkurugenzi wa Taasisi ya Zanzibar Youth Foram, alisema ni vyema kifungu hicho cha sheria kiweke wazi ni yapi maneno ya uchochezi ili kuwapo uhuru wa kutoa habari katika vyombo vya habari.

"Unaposema uchochezi yawezekana kwako wewe ikawa hivyo lakini kwangu mimi ikawa si uchochezi, hivyo ni vyema sheria hiyo kufanyiwa marekebisho ili kuondosha utata uliopo," alisema Maulid.

Jabir Idrisa, mwandishi wa habari mwandamizi, alisema ni vyema kifungu hicho cha sheria kufutwa ili kuondoa hofu kwa waandishi wa habari katika kufanya kazi zao.

Alisema sheria hiyo ina mitego na inaleta hofu kwa waandishi wa habari kutofanya kazi zao vizuri. Alisema sheria hiyo inaeleza uchochezi na ghasia lakini haikuweka bayana ni mazingira yapi ambayo utatumia maneno gani unafanya uchochezi.

"Tunapendekeza kifungu hiki kifutwe kabisa ili kuwa na kifungu kinachokubaliana na maamuru ya katiba ambayo yanatoa haki za msingi ikiwemo haki ya mwananchi kupata habari na haki ya mwanahabari kukusanya na kuchakata habari kwa ajili ya umma," alisema Jabir.

Shadida Omar kutoka Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu, alisema sheria hiyo inakinzana na uhuru wa habari na waandishi wa habari wanafanya kazi kwa maslahi ya jamii, hivyo kifungu hicho kinaweza kuleta athari kubwa.

Alisema kuondolewa kwa kifungu hicho cha sheria, kutapunguza athari na kutolea mfano kuwa mwandishi wa habari anaweza kuonywa huku taasisi yake ikiendelea kufanya kazi. Lakini alisema uwapo wa kifungu hicho unafunga taasisi nzima ya kihabari endapo mwandishi atatoa taarifa inayodaiwa kuwa ni uchochezi.

Jamila Mahamoud, Mkurugenzi wa Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar, alisema kifungu hicho cha sheria kisiondoshwe bali kiwe na ufafanuzi ni upi uchochezi kwa sababu kutokuwa na uhuru usio na mipaka kuna athari zake.

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema Zanzibar inapaswa kuendana na mikataba ya kikanda na kimataifa ambayo ipo inayozungumzia kukuza haki za kibinadamu na uhuru wa habari.

Alisema azimio kubwa ni Azimio la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa la mwaka 1948 ambalo limeweka misingi mikubwa na limezungumza kila mmoja ana haki ya kutoa maoni na kujieleza bila kuingiliwa.

# Mwafaka wafikiwa chaneli zote sasa ZBC

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAJADILIANO ya muda mrefu kuhusu utoaji wa huduma wa maudhui kwa ZBC TV kuwa ni miongoni mwa chaneli za lazima kwa ving'amuzi vyote vya Tanzania limepatiwa ufumbuzi.

Hali hiyo imefikiwa baada ya kufanyika kwa kikao cha mwisho cha majadiliano hayo kati ya watoa huduma wa usambazaji wa maudhui na viongozi wa serikali ya Zanzibar na ile ya Muungano.

Kikao hicho cha majadiliano kilifanyika jana mjini Zanzibar na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa SMT na SMZ wakiwamo Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) na Msemaji Mkuu wa Serikali ya Tanzania, Gerson Msigwa, na Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Fatma Rajab.

Katika kikao hicho, wamekubaliana ifikapo Aprili 26, mwaka huu, chaneli ya ZBC TV kuanza kuoneshwa bure katika ving'amuzi vyote kama ilivyo kwa TBC.

Akifunga kikao hicho Katibu Mkuu Fatma alisema hatua hiyo ni muhimu na itasaidia umoja na ushirikiano kati ya pande mbili za Muungano katika masuala ya habari na mawasiliano.

"Nashukuru sana kwa kukubali kwenu kuwa ZBC sasa inaenda kuonekana katika ving'amuzi vyote Tanzania bila malipo. Kwa kweli leo (jana) tumeandika historia mpya kwa sababu ndani ya miaka 10 mwafaka huu umepatikana," alisema.

Pia alisema hatua hiyo ni moja ya kutekeleza kwa vitendo Muungano wa Tanzania, hivyo kuendelea kushikamana na kufanya kazi kwa pamoja kati ya pande mbili hizo.

Katibu Mkuu huyo aliahidi kuwa wizara yake itaendelea kuwa karibu na watoa huduma wa maudhui ili kutatua changamoto zinapojitokeza.

Msigwa alisema watoa huduma hao wamekubali kutekeleza jukumu la kutambua umuhimu wa ZBC kuonekana bure kupitia ving'amuzi kama ilivyo kwa TBC na kwamba hatua hiyo itakata kiu ya muda mrefu na jambo hilo limekuwa katika majadiliano tokea mwaka 2015 na sasa litaleta mchango mkubwa kwenye utangazaji katika Muungano.

Wakizungumza katika kikao hicho, watoa huduma wa usambazaji wa maudhui walisema hatua hiyo itaongeza ufanisi katika kuwahudumia watanzania katika sekta ya habari na mawasiliano na sekta hiyo kukua zaidi.

Yahya Mohammed, mmoja wa watoa huduma hiyo, alisema kilio chao kikubwa ni kuendelea kupanda kwa gharama za uendeshaji na kutoa huduma kwa Watanzania na kilio hicho ni cha muda mrefu, hivyo umefika muda mwafaka wa kutatuliwa kwa changamoto hiyo.

"Imefika wakati mwafaka sasa kutoka hatua moja kwenda nyingine na kufanya hivyo tunaamini sekta hii itaendelea kuboreka na kodi inayokusanywa kupitia huduma tunazozitoa itaendelea kukua na mwisho wa siku huduma tunazowapelekea Watanzania kupitia makusanyo ya kodi kuendelea kuimarika na kuwa na nchi yenye furaha kwa pande mbili za Muungnao," alisema Yahya.

Kikao hicho cha majadiliano kiliandaliwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kushirikiana na Tume ya Utangazaji Zanzibar.



Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi (wa pili kulia) na Mke wa Makamo wa Pili wa Rais mstaafu wa Zanzibar, Mama Asha Iddi (wa pili kushoto), Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma (kulia) na Mtoto wa Rais wa Zanzibar, Jamila Hussein Mwinyi, wakipata futari iliyoandaliwa na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi (hayupi pichani), Wilaya ya Kaskazini "A" juzi. **PICHA: IKULU**

# Waziri asisitiza mfumo digitali kwa uchumi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema mfumo wa kidigitali ni muhimu katika mageuzi ya kiuchumi na uendeshaji wa biashara.

Aliyasema hayo jana mjini Zanzibar katika hafla ya kuutambulisha mfumo wa kisasa wa kufanya miamala ya kifedha kwa njia ya mtandao kupitia kampuni ya Airpay kutoka India. Soraga alisema hatua hiyo itasaidia kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi kutokana na kuingia katika mfumo huo wa kisasa.

Alisema hivi sasa dunia inakwenda na mabadiliko, hivyo kuwapo kwa mfumo huo kutasaidia kuitangaza Zanzibar kiuwekezaji na kuwa kitovu cha teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kwa nchi za Afrika. Kwa mujibu wa Waziri, mfumo huo wa kifedha utawajali wafanyabiashara wadogo kuwekeza mapato yao kutokana na kuwa uko katika hali ya usalama zaidi.

"Hatua hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha uchumi wa nchi kwa sababu utakuwa mnyororo wa kuwaunganisha wafanyabiashara, wajasiriamali na wawekezaji katika harakati zao mbalimbali za biashara," alisema Waziri Soraga.

Kamishna wa Idara ya Ushirikiano kati ya sekta za umma na binafsi (PPP), Dk. Bill Kiwia, alisema mfumo huo wa Airpay utaifungua Zanzibar kwa upande wa uwekezaji na kuitangaza nje ya Tanzania.

Alisema lazima kwenda na wakati kutokana na mabadiliko ya dunia hakuna kutumia pesa mkononi na badala yake unatumia njia ya mtandao ambayo imerahisishwa kwa wakati huu.

Katika kufikia malengo ya dunia hivi sasa, alisema uchumi wote unaendeshwa na mambo ya TEHEMA na Zanzibar ikiwa moja ya sehemu ya dunia, itanufaika zaidi na mfumo huo.

Meneja wa Airpay, Kunal Kuvnjmunwala, alisema mfumo huo kwa upande wa Afrika utaanza Zanzibar kutoa huduma na kuifanya Zanzibar kuwa sehemu salama katika mambo ya tehama katika uchumi.

Alisema kampuni hiyo ina ubora wa kutoa huduma zinazokwenda na wakati hasa katika mambo ya kidigitali kwa vile dunia ipo ndani ya mfumo huo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**ESTHER MADUBU** anatangaza kupotea kwa cheti chake cha kidato cha sita chenye index number **S1187-0550** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ST. MARY GORETI SECONDARY SCHOOL,** Mwaka: 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/121541/2023.**

---

**Company No. 56941**

**THE GUINEA COMPANY DECORATION AND DESIGN LIMITED**
**P.O.BOX 16909, ARUSHA, TANZANIA**

**To whom it may concern;**

**RE: NOTICE OF A FINAL GENERAL MEETING**
**(Pursuant to section 345 (1) of the companies Act [CAP 212 R.E 2002]**

**PLEASE TAKE NOTICE** that a final General Meeting of the company is to be called on 29th April, 2023 at 02:30pm at the Registered Office of the company at plot Number 255, 257 Block A, House Number 255,257 Ngaresero Road, USA RIVER in Arumeru District for the Liquidator to make an account of the winding up of the Company, showing how the winding up has been conducted, the property of the company in which he dispose of if any and giving explanations to any matter pertaining to winding up of the Company thereto.

**Dated at Arusha this 29th March, 2023**

**Liquidator of the Company**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ISACK P MWANILWA**
ANATANGAZA kupotelewa na kadi ZA PIKIPIKI Zenye namba za usajili **MC 362 ASF, MC 109 ACH na T 524 BNX.**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi
taarifa ya polisi RB namba
**IRI/IRI/RB/118811/2023.**
**AU**
**IRI/IRI/RB/118807/2023.**
**AU**
**IRI/IRI/RB/118814/2023.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**PHILIPO ELIASI NYASTA**
anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **KING LION** yenye jina la umiliki **KINGLION INVESTMENT COMPANY LIMITED** yenye usajili namba **MC251CNB**, CHASSIS NAMBA: **LEAPCK0E2KK0K2433** NA ENGINE NAMBA: **162FMJK0CK2433.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/13096/2022**

---

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

# ***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie: 0782253676***

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Donald Trump akana mashtaka 34 kortini

**NEWYORK,** Marekani

RAIS wa zamani wa Marekani Donald Trump, amejitetea kwa kueleza mashtaka aliyofunguliwa na waendesha mashtaka sawa na kuitusi nchi hiyo.

Kiongozi huyo alifikishwa mahakamani kwa mashtaka ya kumlipa mwanamke mmoja nyota wa filamu za ngono kabla ya uchaguzi, ili asizungumzie uhusiano waliokua nao. Kauli hiyo aliitoa muda mfupi baada ya kuwasili katika makazi yake ya Mar-a-Lago, katika jimbo la Florida, baada ya kurudi kutoka New York kusikiliza kesi yake kwa mara ya kwanza.

Trump alihutubia umati wa wafadhili, marafiki na wafuasi wake, akieleza hakudhani kwamba mtu kama yeye kufunguliwa mashtaka, ni jambo ambalo lingewahi kutokea nchini Marekani.

Trump alijitetea akisema hajafanya kosa lolote na kwamba mashtaka dhidi yake yanastahili kuondolewa mara moja.

**Trump alihutubia umati wa wafadhili, marafiki na wafuasi wake, akieleza hakudhani kwamba mtu kama yeye kufunguliwa mashtaka, ni jambo ambalo lingewahi kutokea nchini Marekani.**

Alidai kuwa kosa lake kubwa lilikuwa kuitetea Marekani kutoka kwa wale wanaonuia kuiharibu.

"Kuanzia mwanzo Wademocrat walikuwa wanachunguza kampeni yangu, mnakumbuka? Walinishambulia kwa kufanya uchunguzi wa uongo, Russia, Ukraine, uongo wa kwanza wa kuniondoa madarakani, uongo wa pili wa kuniondoa madarakani, uvamizi wa makaazi yake ya Mar-a-lago hapa," alisema Trump.

Rais huyo wa zamani ambaye anapigiwa upatu kuipeperusha bendera ya chama cha Republican katika kuwania urais kwenye uchaguzi wa mwaka 2024, alisema waendesha mashtaka nchini humo wanatumia kila mbinu ili wampate na hatia.

Alimshambulia mwendesha mashtaka wa Manhattan. Alvin Bragg, ambaye anaiongoza kesi hiyo akisema hajui lolote kumhusu yeye na jaji anayeisikiliza hiyo kesi Juan Merchan, anayemchukia.

Saa chache kabla ya mkutano huo, alikanusha mashtaka 34 dhidi yake katika mahakama ya New York, katika tukio ambalo lilikuwa la kihistoria kwa rais wa kwanza wa zamani Marekani kufunguliwa mashtaka ya jinai.

Waendesha mashtaka walisema Trump alidanganya mara kadhaa kuhusu rekodi zake za biashara mjini New York, ili kuficha taarifa ambazo zingemchafulia jina kwa wapiga kura katika uchaguzi wa mwaka 2016 ambao alishinda.

Jaji Juan Merchan, alisema kesi hiyo itasikilizwa tena Desemba 4,mwaka huu ingawa wanasheria wanadai huenda hata mwaka ukaisha kabla haijasikilizwa. Wanasheria hao walisema kufunguliwa mashtaka au hata kuhukumiwa, kisheria hakutomzuia Trump kugombea kiti cha urais. **DW**



Maofisa wa polisi wa Israel wakimkamata Mpalestina mmoja wakati vurugu zilipozuka katika eneo la msikiti wa Al-Aqsa Jerusalem jana. **PICHA: AFP**

## Polisi wavamia Al Aqsa

**JERUSALEM,** Israel

POLISI wa Israeli wamewakamata zaidi ya watu 350, baada ya kuzuka kwa makabiliano katika msikiti wa Al-Aqsa mapema jana.

Hayo yamejiri wakati maafisa wa polisi walipoingia kwenye msikiti huo kuwatimua watu waliowaita kuwa wachochezi. Hatua hiyo imeshutumiwa vikali na kundi la Hamas ambalo ni Vuguvugu la Kiislamu la Palestina.

Wanamgambo wa Palestina walijibu uvamizi wa polisi wa Israel kwa kufyatua roketi kuelekea Israel kutoka ukanda wa Gaza, unaodhibitiwa na Hamas.

Hatua iliyosababisha Israel kujibu kwa mashambulizi ya angani.

Vuguvugu la Hamas linalodhibiti Ukanda wa Gaza, limewataka Wapalestina walioko ukingo wa Magharibi kwenda kwa wingi katika msikiti wa Al-Aqsa kwa kile walichosema ni kuulinda msikiti huo.

Hata hivyo, polisi ya Israel ilisema maofisa wake waliingia ndani ya msikiti huo kuwaondoa wale waliowataja kuwa wachochezi, waliojifungia ndani wakiwa na fataki, fimbo na mawe.

Polisi imeongeza kuwa waliwakamata zaidi ya watu 350.

Kwa muda mrefu, msikiti wa Al-Aqsa ulioko mashariki mwa mji mkongwe wa Jerusalem, umekuwa kitovu cha mvutano kati ya Wapalestina na vikosi vya usalama vya Israel. **DW**



# Odinga atishia kurudi barabarani

**NAIROBI,** Kenya


KIONGOZI wa upinzani nchini Kenya, Raila Odinga, ametishia kuanzisha tena maandamano dhidi ya serikali iwapo serikali ya Rais William Ruto, itashindwa kushughulikia masuala yanayolalamikiwa na wananchi.

Odinga alisitisha maandamano na kukubali kufanya mazungumzo na Rais Ruto.

Akizungumza juzi, alisema kauli ya Rais Ruto aliyoitoa mwishoni mwa wiki iliyopita, alipomtaka kusitisha maandamano ya kupinga serikali nchini kote, haikugusia matakwa yaliyotolewa na upinzani.

Rais Ruto alitoa wito wa mazungumzo ya pande mbili bungeni kuhusu kuundwa upya kwa tume ya uchaguzi, lakini hakugusia jinsi serikali yake inanuia kukabiliana na gharama ya juu ya maisha nchini.

Odinga alitaka serikali ichukue hatua za haraka kupunguza gharama ya maisha na pia kupanua mazungumzo yao zaidi.



Alisema, mchakato wa bunge hauwezi kushughulikia matatizo yao na kupendekeza kuundwa kwa timu sawa na Mkataba wa Kitaifa wa 2008, ambao ulisimamiwa na aliyekuwa katibu mkuu wa Umoja wa Mataifa, Koffi Annan.

"Tunawahakikishia watu wetu na Wakenya kwamba macho yetu yameelekeza kwenye mpira, na tunasisitiza kwamba tutarejea kwa watu mapema kabisa kukiwa na ukosefu wa umakini kwa upande mwingine," alisema Odinga.

Odinga pia alidai kulikuwa na majaribio ya kuvuruga seva za uchaguzi, ambazo anataka zikaguliwe tena.

Akizungumza nchini Rwanda ambako anafanya ziara ya kikazi, Rais Ruto alifutilia mbali uwezekano wa kuwepo kwa makubaliano yoyote yatakayoshirikisha upinzani ndani ya serikali yake.

Odinga alikuwa ameitisha maandamano mara mbili kwa wiki baada ya kukataa matokeo ya uchaguzi wa mwaka jana na kukosoa jinsi serikali inavyoshughulikia mzozo wa gharama ya maisha. **BBC**

## Russia yazidi kubanwa

**HELSINKI,** Finland

FINLAND imekuwa mwanachama wa 31 wa muungano wa kujilinda wa Nato, na kuongeza mara mbili urefu wa mipaka ya nchi wanachama na Russia.

Waziri wa mambo ya nje wa Finland, alikabidhi hati ya kujiunga na Muungano huo kwa waziri wa mambo ya nje wa Marekani ambaye aliitangaza Finland kuwa mwanachama.

Baada ya makabidhiano hayo mbele ya makao makuu mapya ya Nato, bendera ya Finland yenye rangi nyeupe na samawati iliwekwa katika bendera nyingine 30.

Kujiunga kwa nchi hiyo ni pigo kwa Rais wa Russia, Vladimir Putin, ambaye alikuwa akilalamika mara kwa mara juu ya upanuzi wa Nato kabla ya uvamizi kamili ndani ya Ukraine.

Msemaji wa Kremlin Dmitry Peskov, alionya kwamba Russia itatazama kwa karibu kile kinachotokea nchini Finland, akielezea upanuzi wa Nato kama ukiukaji wa usalama na maslahi ya kitaifa. **BBC**

# FAINALI LIGI YA MABINGWA MIKOA KUFANYIKA APR 19

**Na Adam Fungamwango**

FAINALI za Ligi ya Mabingwa wa Mikoa 2023 zinatarajiwa kufanyika mkoani Kilimanjaro kuanzia Aprili 19 hadi 28, huku timu nane zikifuzu hatua hiyo, ikiwemo Malimao FC ya Katavi, iliyobugizwa mabao 9-0 na ya Azam FC kwenye Kombe la FA, Desemba 9 mwaka jana.

Taarifa iliyotolewa jana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania, TFF kupitia kwa msemaji wake, Cliford Ndimbo ilisema timu hizo nane zimepatikana kutoka kwenye makundi A hadi D yaliyokuwa yakicheza mechi zake kwa mtindo wa ligi kwenye mikoa ya Shinyanga, Katavi, Kagera na Kigoma na timu mbili za juu zilizoongoza makundi hayo ndizo zilizofuzu.

Timu zilizofuzu kutoka Kundi A ni Nyumbu FC ya Pwani na Mapinduzi FC ya Mwanza, kundi B likitoa timu ya Tanesco FC ya Kilimanjaro na Kiluvya FC ya Dar es Salaam, Kundi C, ipo Navy ya Dar es Salaam na Anuary FC ya Shinyanga, huku Malimao FC ya Katavi na Ilula Tigers ya Iringa zikitoka kwenye Kundi D.

**Malimao imekuwa timu maarufu nchini na ilijulikana baada ya kucheza dhidi ya Azam FC mechi ya raundi ya pili ya Kombe la FA na kutandikwa mabao 9-0 kwenye Uwanja wa Azam Complex.**

Taarifa hiyo ilisema timu zote zinatakiwa kuripoti kituoni Aprili 17 kwa ajili ya kukamilisha taratibu za kushiriki fainali hizo pamoja na kushuhudia droo ya upangaji ratiba.

Baada ya droo, timu hizo zitacheza mechi kwa mtindo wa mtoano na kubaki timu mbili ambazo zitacheza fainali, lakini timu hizo zitakazocheza fainali zitakuwa tayari zimepanda daraja na kucheza Ligi Daraja la Pili kwa msimu wa 2023/24.




Wapiga magita wa bendi ya Sikinde Original wakiwa kazini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Sikinde Original wakamilisha nne mpya*

**Na Sabato Kasika**

BENDI mpya ya Sikinde Original ambayo imezaliwa kutoka ubavuni mwa bendi ya Mlimani Park Orchestra, imekamilisha nyimbo nne za 'Mchepuko, Hila za Ndugu, Tonge la Mwisho na Moyo.

Kiongozi wa bendi hiyo Abdallah , alisema tayari wimbo wa Mchepuko wameshafanyia video huku wakijipanga kuendelea na nyingine zaidi ili kuhakikisha zote zinakuwa katika video.

"Lakini tunaendelea kujipanga ili bendi yetu iweze kusimama yenyewe kwa kuwa na vyombo vyake vya muziki badala kutumia vya kukodi kama ambavyo tumekuwa tukifanya," alisema Hemba.

Hemba alifafanua kuwa wana mkakati wa kuleta vyombo vya muziki kutoka nchini Japan kwa kumtumia mwanamuziki mwenzao, Fresh Jumbe.

"Jumbe anafanya shughuli zake za muziki nchini Japan, lakini pia ni mmoja wanamuziki wa bendi hii, ameondoka kurudi huko kuangalia uwezekano wa kutuma vyombo kwa njia ya ndege au meli," alisema.

Alisema wakati wakisubiri vyombo, wanaendelea kujipanga kwa kuandaa nyimbo, kurekodi na kushuti video ili kusaidia kuitambulisha bendi hiyo ambayo ilianzishwa mwaka jana.

"Wapo baadhi ya watu wamekuwa wakiitabiria kifo bendi yetu, eti kwa sababu inatumia vyombo vya kukodi, lakini ninawaambia kuwa tuko imara hatukuanzisha bendi hii kwa kukurupuka," alisema.

Kiongozi huyo aliwataja baadhi ya wanamuziki wanaounda bendi hiyo kuwa ni Beno Villa, Mjusi Shemboza, Adolph Mbinga na Mbaraka Othman pamoja na Jumbe ambaye anafanya shughuli zake nchi Japan.

## Singida Big Stars yajipanga kupiga yoyote nusu fainali FA

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho (FA), Kocha Mkuu wa Singida Big Stars, Hans Van Pluijm amesema hawahofii timu yeyote watakayokutana nayo kwenye hatua ya nusu fainali.

Singida imefanikiwa kutinga hatua hiyo baada ya kuifunga Mbeya City na sasa inasubiri mshindi wa mchezo kati ya Yanga na Geita Gold FC.

Akizungumza na gazeti hili jana, Pluijm alisema malengo yao makubwa yaliyobakia kwa sasa ni kushinda zilizopo mbele yao na wamejipanga kucheza fainali.

Alisema sasa wanasubiri mpinzani wao na malengo yao msimu huu ni kucheza fainali na ikiwezeka kuwa mabingwa wa michuano hiyo bila ya kujali watacheza na timu gani.

"Mechi yetu na Mbeya City tulikuwa bora kwenye kipindi cha kwanza, lakini kipindi cha pili hatukucheza vizuri kwa kuwa tulikuwa mbele kwa mabao hayo matatu vijana wangu walicheza vizuri na kupambana," alisema Pluijm.

Alisema ameyaona mapungufu kwenye mechi hiyo na atayafanyia kazi kwa ajili ya nusu fainali ya FA na kuwa tayari kukutana na timu yoyote.

## Baleke: Nimejitoa kuisaidia Simba

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Simba, Jean Baleke amesema kwa hatua waliyofikia bado wana kazi kubwa iliyopo mbele yao na wanatakiwa kuendelea kupambana kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika (CAF).

Baleke alisajiliwa na Simba katika kipindi cha dirisha dogo na tayari amesaidia timu hiyo katika Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kutikisa nyavu mara tano na tatu katika ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Baleke alisema anatambua wanaenda katika hatua ngumu ya robo fainali na kulazimika kupata matokeo mazuri ili kusonga mbele.

Alisema, michuano hiyo inawakutanisha na wachezaji wenye viwango tofauti na wanaocheza ligi tofauti hivyo watakuwa na mengi ya kujifunza kutoka kwao.

"Kufunga ni jukumu langu kila ninapopata nafasi ya kufanya hivyo, maana yangu ni kwamba tunacheza watu wengi uwanjani nikiona mchezaji mwenzangu yupo nafasi ya kufunga natoa pasi wote tunajenga Simba moja."

Alisema hatakiwi kuwa mchoyo kwa mchezaji mwenzake anapokuwa katika nafasi nzuri ya kuweza kusaidia timu kupata ushindi kwa sababu ana imani kubwa ya wachezaji walikuwapo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CHELSEA YATAJA MAKOCHA

KLABU ya Chelsea imefanya mawasiliano na kocha wa zamani wa Bayern Munich, Julian Nagelsmann, 35 na kocha wa zamani wa Hispania, Luis Enrique, 52, juu ya kuwa kocha mpya wa klabu hiyo. ***(Telegraph)***

### ZERBI HATARAJIWI

BOSI wa Brighton, Roberto de Zerbi, 43, hatachukuliwa kuwa kocha anayetarajiwa wa Chelsea baada ya kutimuliwa kwa Graham Potter. ***(Subscription Required)***

### POTTER KUMRITHI MOYES

GRAHAM Potter, 47, anawania kuwa kocha anayefuata wa West Ham huku klabu hiyo ikitarajiwa kufikiria mustakabali wa kocha wa sasa, Scot David Moyes, 59, msimu wa joto. ***(Telegraph)***

### VIEIRA KOCHA MPYA FOREST

KOCHA wa zamani wa Crystal Palace, Patrick Vieira mwenye umri wa miaka 46 anaweza kuwa kocha wa Nottingham Forest ikiwa klabu hiyo itaamua kumfukuza, Steve Cooper, 43. ***(Mail)***

### MESSI NA PSG

MSHAMBULIAJI wa Argentina, Lionel Messi, 35, huenda asifikie makubaliano na Paris St-Germain ya kuongeza muda wake wa kukaa kwenye klabu hiyo. ***(ESPN)***

### AL-HILAL YATOA OFA

KLABU ya Al-Hilal ya Saudi Arabia imetoa ofa rasmi kwa Lionel Messi ya mshahara wa euro milioni 400 kwa mwaka. ***(Fabrizio Romano)***

### MIN-JAE AGOMBEWA

KLABU za Manchester United, Liverpool na Tottenham Hotspur zimeonesha nia ya kuamsha kifungu cha pauni milioni 40 cha kumtoa beki wa Napoli na Korea Kusini, Kim Min-jae, 26. ***(Mail)***

### CAICEDO ATAKIWA

LIVERPOOL imeelekeza mawazo yake kwa kiungo wa kati wa Brighton na Ecuador, Moises Caicedo, 21, baada ya Wolves kuondoa kipengele kutoka kwa kiungo wa kati wa Ureno, Matheus Nunes, 24, ambacho kingewaruhusu Wekundu hao kufanya ununuzi wa kumnunua mchezaji huyo kwa pauni milioni 44 msimu huu. ***(Mirror)***

### CEBALLOS AWANIWA

KLABU ya Wolves inajiandaa kumnunua kiungo wa kati wa Real Madrid na Hispania, Dani Ceballos, 26, huku mkataba wa mchezaji huyo ukimalizika msimu huu. ***(9min)***


### DE BEEK KUREJEE

KLABU ya Ajax ina nia ya kumrejesha kiungo wa kati wa Manchester United na Uholanzi, Donny van de Beek, 25, katika klabu hiyo msimu huu. ***(Football Insider)***

### VLAHOVIC HUYO ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Serbia, Dusan Vlahovic, 23, atakuwa tayari kujiunga na Arsenal msimu huu wa joto. ***(Four Four Two)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# TEN ATAKA MAN UTD ICHEZE KAMA ROBOTI

**Nia ni kutaka kurudi kwenye ubora wao ili kufuzu ligi ya mabingwa Ulaya na...**

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag anajua kuwa wachezaji wa Manchester United ni binadamu tu, lakini anahisi lazima "wafanye kama roboti" ili kupata matokeo mazuri.

**United iliteleza kwa kichapo cha mabao 2-0 katika mechi yao ya kurejea Ligi Kuu Jumapili dhidi ya wapinzani wao walio katika nafasi ya nne bora Newcastle United.**

Ingawa wameonesha kiwango cha juu katika Kombe la FA na Ligi ya Europa, pointi moja pekee kutoka mechi tatu za mwisho za ligi kuu imewafanya wabaki nafasi ya tano kwenye msimamo.

Hata hivyo, Ten Hag hana shaka na kikosi chake kwani kinaweza kurudisha ubora wao.

"Ninakubali tunarudi kwenye tabia za zamani, lakini najua kuna mabadiliko," alisema akiiambia The Guardian.

"Wachezaji sio roboti. Lakini inabidi tufanye kama roboti, kama mashine. "Lazima tutarajie na kuwataka wachezaji wetu walingane na viwango hivyo, tusipofanya hivyo tunasikitishwa kwa sababu hiyo ni kazi yetu.

"Tumeonesha katika michezo mingi kwamba tunaweza kufanya hivyo. Ilikuwa imani ngumu na yenye nguvu sana.

"Tumeonesha katika michezo mingi. Tumeonesha tunaweza kushinda michezo, lakini unapaswa kufanya hivyo katika kila mchezo kwa sababu hilo ni hitaji la Manchester United."

United inaweza kujivuta katika nafasi za kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya kama jana Jumatano ilishinda dhidi ya Tottenham Hotspur iliyo nafasi ya nne.

Ten Hag pia atakuwa na jicho moja la kurejea kwenye michuano ya Ligi ya Europa wiki ijayo, huku klabu hiyo ikitarajiwa kuwakaribisha Sevilla wiki moja siku ya Alhamisi katika mchezo wa mkondo wa kwanza wa robo fainali.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,099,1

MECHI KALI

FENERBAHCE
VERSUS
KAYSERISPOR

1 | 1.40
X | 4.46
2 | 6.22

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom | m-pesa
halopesa
airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# WACHUANA KUMRITHI POTTER



**LONDON,** England

CHELSEA inawasiliana na Julian Nagelsmann na Luis Enrique huku wakiongeza kasi ya kutafuta mbadala wa Graham Potter, huku The Blues hao pia wakitarajiwa kuzungumza na Mauricio Pochettino.

Nagelsmann na Enrique, ambao wote hawana kazi, ni wawili kati ya wagombea wakuu wa kurithi mikoba ya Potter baada ya kufuatia kutimuliwa kwake baada ya chini ya miezi saba kuwaongoza Blues hao.

Chelsea iko tayari kufikiria wagombea saba kabla ya kufupisha orodha hiyo katika msako unaoongozwa na wakurugenzi wa michezo, Paul Winstanley na Laurence Stewart.

Nagelsmann anafahamika kwa Stewart na mkurugenzi wa ufundi wa klabu hiyo Christopher Vivell, baada ya kufanya kazi na wote wawili kule RB Leipzig.

Nagelsmann mwenye umri wa miaka 35 ana nia ya kuelewa zaidi kuhusu klabu, muundo wake na kiwango cha ushawishi ambacho angeweza kuwa nacho.

Nagelsmann pia anatajwa na klabu nyingine ikiwepo Real Madrid pamoja na Tottenham.

Enrique aliondoka kama kocha mkuu wa Hispania mkataba wake ulipomalizika baada ya Kombe la Dunia Desemba mwaka jana.



## Kocha ajivunia kiwango Chelsea

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa muda wa Chelsea, Bruno Saltor alipongeza kiwango cha wachezaji wake baada ya kutoka suluhu na Liverpool, Jumanne.

Chelsea walipoteza nafasi kadhaa za wazi za kushinda mechi yao ya kwanza tangu Graham Potter atimuliwe, huku Kai Havertz akinyimwa bao kipindi cha pili na VAR.

Matokeo hayo yameifanya The Blues kubaki nafasi ya 11 kwenye msimamo wa Ligi Kuu, lakini kulikuwa na sababu ya kuwa na matumaini baada ya mchezo ambao Liverpool walifanikiwa kupiga mashuti mawili pekee kutoka ndani ya eneo la wapinzani wao.

Akizungumzia sare hiyo, Bruno ambaye ni mlinzi wa zamani wa Brighton and Hove Albion alielezea fahari yake katika uchezaji wa Chelsea, licha ya kushindwa kufunga katika mechi ya sita tofauti za ligi nyumbani msimu huu.

"Niliwaomba wachezaji wacheze kwa mioyo yao na nadhani tuliona hilo," alisema kocha huyo raia wa Hispania akiiambia Sky Sports.

"Tulitoa kila kitu, tulitengeneza nafasi. Tu funga mara mbili, moja kuotea na moja la mkon

"Nadhani ilikuw utendaji mzuri kutok kwa vijana, ni mwanz mzuri kwao baada ya sik ngumu na zenye hisia.

"Waliweza kujiwel wazi, kutumia vichw vyao na mioyo yao pi hivyo sifa kwao.

"Umekuwa msim mgumu sana kwao. Kur jea kutoka kwa haba tulizokuwa nazo sik chache zilizopita ni jamb la ajabu.

"Inaonesha kuwa w naweza kuzingatia waka huu na kufanya vyem Wanapaswa kujivunia."

164,188/-

# MECKY MEXIME AIPIGIA HESABU YANGA LIGI KUU

Na Hadija Mngwai

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Mexime aipigia hesabu kali Yanga katika mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa Aprili 11 kuhakikisha anaibuka na alama tatu.

Kagera Sugar ipo nafasi ya saba ya msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 32 ambapo inatarajia kuvaana na Yanga Aprili 11 katika mchezo wa Ligi Kuu Bara.

**Akizungumza na Nipashe, Mexime amesema kuwa, kikosi chake kipo vyema hivyo anajipanga kuikabili Yanga Aprili 11 ili kuweza kutwaa pointi tatu.**

"Mchezo wetu unaofuata tunacheza na Yanga, siku zimeshakwisha hakuna muda wa kupumzika, tunahitaji kujiandaa ili kuweza kufanikiwa kutwaa alama tatu.

" Ligi ni ngumu na ina ushindani mkubwa hasa mechi hizi za mwisho kila timu inapambana kupata matokeo hivyo tunajipanga kuweza kupata matokeo mazuri," alisema Mexime.

Aidha, alimalizia kwa kusema kuwa, kikosi chake kipo vizuri hivyo wanajipanga kumaliza vizuri.

Ligi Kuu Bara ipo ukingoni ambapo kila timu imebakiza michezo mitano ili kukamilisha msimu wa 2022/23.

## Yanga SC yajivunia rekodi, msimu bora

INATOKA UK. 24

timu hiyo ina kocha mzuri na wachezaji wake wana viwango vikubwa.

"Lakini sisi lengo letu kama nilivyosema msimu huu ni wa mafanikio ya kuchukua Ubingwa wa Tanzania Bara, Kombe la FA, halafu tupo kwenye robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, huko nako tunataka kufanya vizuri," alisema Kamwe.

Msimu huu Yanga imetolewa kwenye michuani miwili tu kati ya mitano ambayo imeshiriki ambayo ni Kombe la Mapinduzi na Ligi ya Mabingwa Afrika ilipoodolewa kwa jumla ya mabao 2-1 na Al Hilal ya Sudan na kuangukia kwenye Kombe la Shirikisho ambapo ilifanikiwa kuiondoa Club Africain ya Tunisia kwenye hatua ya mchujo, kabla ya kutinga hatua ya makundi na sasa robo fainali.



Vijana wakicheza mpira wa Kikapu katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Simba yawapiga 'stop' Akpan, Okwa, Ihefu

INATOKA UKURASA 24

ba na ipo duniani kote, kwa maana hiyo sisi kwa Akpan na Okwa hawatocheza kwenye mechi zote ambazo Ihefu watacheza dhidi yetu."

Simba ambayo ilianza mazoezi Jumanne iliyopita mara baada ya kurejea kutoka nchini Morocco ilikokwenda kucheza mechi ya kukamilisha ratiba ya Ligi la Mabingwa Afrika Kundi C dhidi ya Raja Casablanca, itarudiana na Ihefu kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam na mshindi wa mechi hiyo atacheza na Azam FC ambayo imetinga hatua ya nusu fainali baada ya kuifunga Mtibwa Sugar mabao 2-0.


# SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 08/04/23 | 17:00 | Fulham FC vs West Ham United | 2.55 | 3.15 | 2.60 |
| 02. 08/04/23 | 17:30 | Sampdoria Genoa vs US Cremonese | 2.24 | 3.10 | 3.10 |
| 03. 08/04/23 | 19:30 | Hellas Verona vs Sassuolo Calcio | 2.50 | 3.10 | 2.70 |
| 04. 08/04/23 | 19:30 | Torino FC vs AS Roma | 3.15 | 2.95 | 2.31 |
| 05. 08/04/23 | 21:45 | Lazio Rome vs Juventus Turin | 2.60 | 2.90 | 2.80 |
| 06. 08/04/23 | 21:45 | KAA Gent vs Union Saint-Gilloise | 2.46 | 3.35 | 2.60 |
| 07. 09/04/23 | 14:00 | Olympique Lyon vs Stade Rennes | 2.25 | 3.30 | 2.90 |
| 08. 09/04/23 | 15:00 | Real Valladolid vs RCD Mallorca | 2.47 | 2.90 | 2.95 |
| 09. 09/04/23 | 15:30 | FC Emmen vs NEC Nijmegen | 2.80 | 3.30 | 2.35 |
| 10. 09/04/23 | 16:00 | AC Ajaccio vs AJ Auxerre | 2.70 | 2.90 | 2.65 |
| 11. 09/04/23 | 16:00 | Montpellier HSC vs Toulouse FC | 2.28 | 3.40 | 2.80 |
| 12. 09/04/23 | 16:00 | ESTAC Troyes vs Clermont Foot 63 | 2.55 | 3.20 | 2.60 |
| 13. 09/04/23 | 16:30 | Borussia Monchengladbach vs VfL Wolfsburg | 2.26 | 3.50 | 2.75 |
| 14. 09/04/23 | 18:30 | Liverpool FC vs Arsenal FC | 2.46 | 3.45 | 2.55 |
| 15. 09/04/23 | 18:30 | VfL Bochum vs VfB Stuttgart | 2.85 | 3.20 | 2.34 |
| 16. 09/04/23 | 19:30 | UD Almeria vs Valencia CF | 2.75 | 3.15 | 2.43 |
| 17. 09/04/23 | 19:30 | Standard Liege vs KRC Genk | 2.70 | 3.45 | 2.32 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## ALHAMISI - 06/04/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3825 | Croydon Kings vs Adelaide Comets | 3.26 | 3.68 | 1.92 |
| 14:00 | 3700 | Skive IK vs AB Gladsaxe | 4.13 | 3.56 | 1.70 |
| 14:00 | 3883 | Dalum vs Middelfart | 21.83 | 8.32 | 1.07 |
| 14:30 | 2831 | Loko Tbilisi vs Gareji | 2.52 | 3.06 | 2.65 |
| 15:00 | 3340 | FC Roskilde vs Thisted FC | 2.39 | 3.43 | 2.50 |
| 15:00 | 4495 | Holstebro vs AB Taarnby | 1.89 | 3.64 | 3.38 |
| 15:15 | 1704 | CLB Viettel vs Hoang Anh Gia Lai | 1.90 | 3.19 | 3.70 |
| 15:30 | 3040 | NK Dubrava vs NK Dugopolje | 1.93 | 3.23 | 3.54 |
| 15:30 | 5618 | Hougang United vs Tanjong Pagar United FC | 1.85 | 3.99 | 3.12 |
| 16:00 | 5015 | Viborg FF vs Aalborg | 1.81 | 3.47 | 3.84 |
| 16:00 | 5057 | Poland W vs Costa Rica W | 1.30 | 4.76 | 8.08 |
| 16:30 | 4399 | Psis Semarang vs PSM Makassar | 3.80 | 3.44 | 1.80 |
| 17:00 | 1055 | Valmiera Fk/Bjss vs FK Tukums 2000/Tss | 1.22 | 5.59 | 9.73 |
| 17:00 | 3443 | NK Rogaska vs NK Bistrica | 1.39 | 4.46 | 6.43 |
| 17:00 | 3503 | FK Radnicki 1923 vs Radnicki Nis | 2.20 | 2.97 | 3.13 |
| 17:00 | 4196 | GKS Jastrzebie Zdroj vs Kotwica Kolobrzeg | 3.04 | 3.25 | 2.16 |
| 17:30 | 3140 | Cibalia Vinkovci vs Bsk Bijelo Brdo | 1.68 | 3.59 | 4.21 |
| 18:00 | 2529 | Silkeborg vs Sonderjyske | 1.54 | 4.04 | 4.87 |
| 18:00 | 3214 | Sepsi Osk vs CS Mioveni | 1.50 | 3.73 | 6.01 |
| 18:30 | 3199 | MES Rafsanjan vs Naft Masjed Soleyman FC | 1.41 | 3.92 | 7.23 |
| 19:00 | 1015 | Persepolis FC vs Malavan Bandar Anzali | 1.39 | 3.75 | 6.40 |
| 19:00 | 1546 | Novi Pazar vs Radnik Surduluca | 1.87 | 3.18 | 3.85 |
| 19:00 | 1730 | Chojnice vs Nieciecza KS | 3.39 | 3.34 | 1.94 |
| 19:00 | 2711 | Pafos FC vs Omonia Nicosia | 1.94 | 3.21 | 3.68 |
| 19:00 | 2770 | Sanat Naft Abadan vs Sanat Mes Kerman FC | 2.75 | 2.65 | 2.55 |
| 19:00 | 3049 | Chrobry Glogow vs Sandecja | 2.58 | 3.09 | 2.51 |
| 19:00 | 3566 | Alessandria vs US Ancona 1905 | 2.98 | 2.87 | 2.59 |
| 19:00 | 4807 | Spain W vs Norway W | 1.83 | 3.37 | 3.88 |
| 19:00 | 5079 | Slask Wroclaw vs GKS Piast Gliwice | 3.15 | 3.04 | 2.16 |
| 19:00 | 5803 | Javor Ivanjica vs Cukaricki St | 3.66 | 3.25 | 1.89 |
| 20:00 | 1135 | FC Krasnodar vs Rostov | 2.00 | 3.42 | 3.26 |
| 20:00 | 2560 | Rot-Weiss Hadamar vs FC 1906 Erlensee | 3.40 | 4.10 | 1.66 |
| 20:00 | 4277 | TSV Steinbach II vs SV 1898 Unter Flockenbach | 2.55 | 4.10 | 2.01 |
| 20:00 | 4793 | SV Steinbach 1920 vs FSV Fernwald | 3.10 | 3.85 | 1.79 |
| 20:00 | 5071 | Eintracht Frankfurt II vs Bayern Alzenau | 1.45 | 4.20 | 4.60 |
| 20:00 | 5534 | Baunatal vs TUS Dietkirchen | 2.10 | 3.95 | 2.70 |
| 20:30 | 3687 | Vejle BK vs Copenhagen | 4.65 | 3.52 | 1.66 |
| 20:30 | 5920 | Fenerbahce vs Kayserispor | 1.40 | 4.46 | 6.22 |
| 21:00 | 1766 | CFR Cluj vs Argesul Pitesti | 1.57 | 3.53 | 5.60 |
| 21:00 | 5090 | US Pergolettese vs Vicenza | 2.64 | 2.87 | 2.92 |
| 21:15 | 3460 | Olimpija Ljubljana vs NK Celje | 2.07 | 3.32 | 3.17 |
| 21:15 | 4297 | Wales W vs Northern Ireland W | 1.27 | 4.96 | 8.89 |
| 21:30 | 2330 | Ruch Chorzow vs Podbeskidzie Bie | 2.24 | 3.09 | 2.93 |
| 21:30 | 4348 | Gornik Zabrze vs Korona Kielce | 1.89 | 3.23 | 3.69 |
| 21:30 | 5491 | Sturm Graz vs LASK Linz | 1.95 | 3.43 | 3.38 |
| 21:30 | 5932 | Czech Republic W vs Morocco W | 1.30 | 4.78 | 8.31 |
| 21:45 | 3204 | Annecy FC vs Toulouse | 4.02 | 3.66 | 1.81 |
| 21:45 | 3526 | England W vs Brazil W | 1.32 | 4.76 | 7.45 |
| 22:00 | 3888 | Al Fateh (KSA) vs Al Khaleej Club | 1.62 | 3.95 | 5.01 |
| 22:15 | 5585 | El Ittihad Alexandria vs Coca Cola | 2.90 | 2.95 | 2.49 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Alhamisi Aprili 6, 2023

Nipashe



**'Man Utd icheze kama roboti'** UKURASA 21



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini. **PICHA: SIMBA**

# Simba yawapiga 'stop' Akpan, Okwa, Ihefu

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Ni kwa sababu za kitaalam ikiwamo upangaji wa matokeo, kwa kuwa...

WAKATI Simba ikitarajiwa kucheza mechi yake ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) dhidi ya Ihefu kesho, klabu hiyo imewapiga 'stop' nyota wake, Nelson Okwa na Victor Akpan ambao wapo kwa mkopo kucheza dhidi yao.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu ya Simba, Ahmed Ally alisema jana kuwa Okwa na Akpan hawatocheza kesho kwenye mechi hiyo kwa sababu ya makubaliano ya mkataba wa mkopo ambayo waliwapa Ihefu.

Alisema siyo kwenye mechi hiyo tu, bali hata mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Aprili 10 kwenye Uwanja wa Highland Estates, Ubaruku, Mbarali, Mbeya.

**"Akpan na Okwa ni wachezaji wetu ambao wapo Ihefu kwa mkopo na kwenye makubaliano yetu ni kwamba hawa tocheza kwenye mechi yoyote dhidi yetu," alisema Ahmed.**

Okwa na Akpan ambao wote ni raia wa Nigeria walipelekwa kwa mkopo kipindi cha dirisha dogo la usajili katika klabu hiyo baada ya kuonekana hawana nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha Simba.

"Kuna mikataba ya aina mbili, ya kumruhusu mchezaji kucheza kwenye timu aliyotoka na upo ambao hamruhusu kuichezea timu ya mkopo dhidi ya timu mama. Na zipo sababu za kitaalam hapo ambazo zinasababisha vitu vyote hivyo ikiwemo upangaji wa matokeo, timu inayommiliki mchezaji ambaye wanamlipa, inaweza kutumia mwanya huo huo kumshawishi, yaani acheze chini ya kiwango kwenye mechi ya timu yake ya mkopo dhidi ya timu yake mama," alisema Ally.

Aliongeza: "Na siyo hivyo kuna mengi tu yaliyo kinyume chake na yanayofanana na hayo, kwa hiyo kuepusha hivyo ndiyo ikaja hiyo mikata-

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga SC yajivunia rekodi, msimu bora

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema inajivunia kuwa na msimu bora zaidi kuwahi kutokea kwenye historia ya klabu hiyo kutokana na mafanikio makubwa iliyoyapata na inayoendelea kuyapata kwenye michuano yote inayocheza hadi sasa.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ally Kamwe alisema Yanga ipo kwenye asilimia nyingi za kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini wanalitafuta Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (FA), lakini pia wametinga hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho na Mpira wa Miguu barani Afrika, CAF.

"Msimu huu umekuwa wa mafanikio kwetu na tumeweka rekodi mbalimbali, kwanza tumekuwa timu ya kwanza Tanzania kuifunga TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo. Pia tumekuwa moja ya timu tatu ambazo zimeifunga TP Mazembe nyumbani na ugenini," alisema.

Aliongeza: "Timu hizo ni sisi wenyewe Yanga, US Monasrtir ya Tunisia msimu huu na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini misimu kadhaa nyumba, zaidi ha hapo hakuna timu yoyote Afrika iliyowahi kufanya hivyo.".

Wakati Yanga ikiweka rekodi hiyo, Kamwe alisema mafanikio iliyoyapata ni kwamba mpaka sasa wapo kwenye michuano mitatu na wanafanya vema.

"Sisi ni mabingwa watetezi na msimu huu tunaendelee kuongoza ligi na tuna asilimia kubwa ya kulichukua taji la Ligi Kuu na lengo ni kuchukua yote pamoja na Kombe la FA. Kumbuka huku kwenye FA tupo hatua ya robo fainali na tunakwenda kucheza Jumamosi dhidi ya Geita Gold, tunajua siyo mechi nyepesi kwa sababu

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >